# ANAYENG'ANG'ANIA

Asante, Ndugu Borders. Mwaweza kuketi. Samahani kwa kuchelewa, lakini nilikuwa, mtoto mdogo mgonjwa, nilikuwa nikijaribu kumhudumia nilipokuja, naye mzazi alikuwapo, alisumbuka sana kuhusu hilo. Na kwa hiyo, nilikuwa nikimwombea mtoto huyo mchanga, na leso ambazo nilikuwa. . .zilikuwa zimeletwa kwangu niziombee. Mnaamini katika huduma hiyo, kuombea. . .? Loo, naam, hakika tunaamini.

2 Sasa, tunaninii. . .kweli tunayahesabu haya kuwa ni majaliwa makubwa kuwa nanyi watu wazuri, hapa kwenye kisiwa hiki juma hili, kutoka kwa ninii yote. . .kutoka Port Alberni na hapa Victoria. Nami nilishukuru sana jana usiku (Moyo wangu uliniuma ndani yangu kwamba tulikuwa na siku tatu tu za kuwa hapa, siku moja zaidi.) nilipoona kilichotokea jana jioni, kuona kundi zima likikiri makosa yao, na kuja na kufanya marekebisho.

3 Sasa hilo—hilo linamaanisha kwamba kuna uwezekano mkubwa wa u—uamsho mkubwa kote katika kisiwa hiki hapa, ambao Mungu angeweza—angeweza, angetujalia. Ninaamini ya kwamba atafanya hivyo kama tutamwamini tu, nasi tuna imani ya kwamba ata—atafanya hivyo.

4 Sasa, ninamshukuru Ndugu Byskal, Eddie, kama nimjuavyo, mvulana wa thamani sana. Nilimpenda sana kijana huyu nilipokutana naye huko. . .huko Dawson Creek. Mara yangu ya kwanza ilikuwa huko Grande Prairie, lakini alikuwa Dawson Creek wakati huo, nami nikakutana naye huko. Naye alikuwa akiniambia ati yeye alikuwa mmishenari kwa Wahindi.

Nami nikasema, "Eddie, na—naja Canada tena moja ya siku hizi, na nitaingia huko, niwaone marafiki zako."

5 Akasema, "Vema tu." Basi akaniambia, kasema, "Baadhi ya ndugu," kasema, "huenda wakapitia Victoria, wazigawanye hizo tarehe kutoka huko juu." Na—naye akasema, "Lakini watakuwa na m—mkutano huko chini, mkutano mkubwa." Nilisikitikia jambo hilo, lakini ninataka kusema, naomba radhi kwa kuingia wakati huo, mimi na Ndugu Borders, na sisi sote. Ikitokea baadhi ya ndugu wawepo, hatukutaka kuingia, au kusaidia, au, kuzuia mkutano wenu mkubwa, bali tu kuwaombea wagonjwa tunapopitia. Nami nataka kusema, mnao watu wazuri. Tumeupenda.

6 Huu ndio mwisho wa ibada kumi na moja mfululizo kwangu bila kupumzika, na karibu nimepwelewa kabisa na sauti. Imepotea sana, mpaka, huu hapa muktadha ambao ningezungumzia alasiri hii: *Kitendawili*, na nikija huko nje,

kitu Fulani kilisema, “Huna sauti ya kulifanya.” Kwa hivyo, nikachagua kitu kingine basi.

7 Hii imekuwa tangu Mei ambapo nimekuwa kwenye mikutano. Nilikuwa Green Bay, Michigan; na kutoka huko hadi Chicago, Illinois; hadi Southern Pines, North Carolina; kule chini Columbia, South Carolina; kuelekea Cow Palace huko Los Angeles. Na kutoka huko hadi Santa Maria, kutoka huko hadi Grass Valley, kutoka Grass Valley hadi Spokane, kutoka Spokane kurudi chini hadi Salem, kutoka Salem mpaka *hapa*, na *hapa*. Mnaona? Ninachoka.

8 Sasa, kuhubiri tu hakunisumbui. Ninapwelewa na sauti kidogo, kwa sababu, nafikiri, kuongea sana. Lakini, maono ndiyo yanayonisumbua. Mojawapo ya hayo ni zaidi ya saa kumi ungehubiri kwa sauti yako yote, moja tu, itakufanyia kiasi hicho.

Ikiwa ndiyo mara ya kwanza kuwa pamoja nanyi, na imani yenu kuu ya kuitikia huo, hakika ninawashukuru. Mungu awabariki daima.

9 Sijui, kulikuwa na matumizi yaliyouhusu huu mkutano, naamini. Nami nikamwambia Eddie, “Ninii tu,” nilipokuja hapa, nilisema, “sasa, Ndugu Eddie, hata usitaje sadaka.” Nikasema, “Ka—kanisa letu la nyumbani litayashughulikia, kwa sababu sisi ni wageni na. . . ” kuyashughulikia. Sasa, nasikia ya kwamba yeye alichukua matoleo, na, ama *kitu kama hicho*, na alitaka kuninii. . .Nami nikasema, “Kama ulifanya hivyo, yatumie tu kwa gharama.” Hatutaacha deni lolote. Hatujafanya hivyo bado.

10 Kamwe hatuamini katika kuwaomba watu pesa. Sisi. . .Ni—nimekuwa katika huduma kwa muda wa miaka thelathini na miwili na sikuwahi kuchukua matoleo maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Wakati. . .Na siku hizi, na—nalipwa kutoka kwa kanisa langu dola mia moja kwa juma, nanyi mnajua jinsi inavyotubidi kuishi kwa hizo.

11 Lakini wazia jambo hilo, Bwana wetu hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Hiyo ni kweli. Mnaona? Kwa hiyo, Yeye alikuwa na vazi moja alipokuwa hapa, mtu fulani alimpa. Na kwa hivyo, sidhani kwamba inafaa, Wakristo kujaribu kujilinganisha na ulimwengu, kuwa, mwajua, “kujigamba,” kama tunavyosema huko Marekani, na kujiinua sana, na kuwa na yaliyo bora zaidi. Mbona, ninaamini sikuzote tunaweza kuchukua yaliyo duni kabisa, ndi—ndiyo njia bora zaidi, Yeye alifanya hivyo, Yeye ni Mungu wa Utukufu, alishuka chini pasipo na mahali pa kulaza kichwa Chake. Na, nadhani hiyo ni, jinsi tunavyotaka kuishi.

12 Na, watu wengi wanajua kwa huduma ya aina hii, jamani, kama ungelikuwa haini, ungeweza kuwa, mbona, ungeweza kuwa milionea. Nami ningeogopa kukuandikia hundi alasiri hii, akaunti yangu binafsi, ya zaidi ya dola mia mbili au tatu. Hakika

ingerudishwa, nawaambia hivyo. Lakini, jambo ni kwamba, hatuko nje hapa kwa ajili ya pesa, tuko hapa nje kujaribu kuusaidia Ufalme.

13 Siko hapa nje kushutumu kanisa lolote, dhehebu lolote, chochote kile. Mara nyingi mnanisikia nikilikemea, lakini si dhehebu ninalokemea, ni hiyo dhambi mle ndani, hiyo ndiyo ninayokemea.

14 Kama nilikuona ukishuka mtoni kwa mashua ndogo, na mashua hiyo ilikuwa inavuja, na kulikuwa na maporomoko makubwa chini yako, mikondo yenye nguvu, nami nilijua mashua hiyo isingeweza kustahimili hayo maporomoko, hiyo mikondo yenye nguvu, huku mimi nakupigia kelele, na kukukemea, na kujaribu kukutoa humo, si kwa sababu sikupendi, ni kwa sababu kweli nakupenda. Na—nawapenda. Mnaona? Imani na upendo hurekebisha. Mnaona? I—inarekebisha.

15 Kama mtoto wako mdogo alikuwa ameketi hapa nje barabarani, nawe unajua msongamano wa magari unapitia hapo, je, ungesema, "Junior, mpenzi, nafikiri unapaswa kuingia ndani"? Hiyo ni karibu kama vile wahudumu wengine wanavyojaribu kurekebisha kusanyiko lao. Mbona, kama ulikuwa ni mama ama baba halisi, ungetoka uende pale na kumwondoa hapo, na kama akitoka tena, ungekuwa na kijiti, wakati mwingine, mkononi mwako, ulipomfuatilia. Hiyo haionyeshi kuwa humpendi huyo mtoto, inaonyesha unampenda huyo mtoto, unajua.

16 Wala, siwakemei ninyi. Najua hiyo mashua haitastahimili hayo mawimbi pale chini nami ninajaribu kukutoa. Hilo ndilo ninalofuatilia. Na hivyo ndivyo ninavyowazia kuhusu madhehebu ya kidini. Si kwamba nina neno dhidi ya hao watu binafsi, ni huo mfumo, mfumo ambao unatenganisha udugu. Wanasema, "Mimi ni Mpresbiteri, wala hatuna uhusiano . . . "

17 Nimekuwa hospitalini na kuanza, katika wodi, na kuanza kuomba. Nikasema, "Je, ninyi watu mnaweza kuinamisha vichwa vyenu?"

"Sisi ni Wamethodisti."

18 Wakati mmoja nilimwambia mwanamke fulani, "Je, wewe ni Mkristo?"

Akasema, "Nataka uelewe mimi huwasha mshumaa kila usiku." Kana kwamba hiyo ina uhusiano wowote na Ukristo.

19 Kisha mmoja akasema, "Ati nini?" Mwanamke mmoja akasema, "Ati Mkristo?" kasema, "Mimi ni Mmarekani." Huo sio ushuhuda mzuri sana kwa Ukristo, nitasema hivyo, na kwa hivyo, hiyo haina uhusiano wowote nayo.

20 Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi hata kuuona," hiyo ni kuuelewa, "Ufalme wa Mungu." Nami

nina bidii sana kwa watu, nina bidii kwa Kanisa. Nami ninapoona yakipotosha, madhehebu yakiwafarakanisha watu na kuwatenganisha, kuwafanya kuwa tofauti, na kisha kundi lilo hilo likawa baridi kwenye Neno la Mungu na kadhalika. Hiyo . . . Sina neno dhidi yao, ninajaribu kuchukua Neno na kulitikisa lirudi pamoja tena.

21 Nilitawazwa wakati mmoja, katika kanisa la Baptisti ya Kimishenari. Ndipo, nilipoitwa kwenye huduma, hapa, kuninii . . . nilininii tu . . . Loo, kwa sababu ya Ba—Baptisti ya Kimishenari, ni . . . si dhehebu, ni ushirika tu, wewe ni mshiriki wake tu. Ni kama isiyo na mipaka ya kimadhehebu. Unaweza kuhubiri chochote utakacho, maadamu unaishi maisha safi, unaweza kuwa Mbaptisti wa Kimishenari. Wewe . . . Utovu wa uadilifu ndio kitu pekee kikuondoacho. Mradi . . . Halafu basi, ubatizo wao, wanaamini ya kwamba maji hukubatiza ukawa mshirika, naye Roho anakubatiza kuwa katika ule Mwili. Na kwa hivyo, basi, haidhuru umebatizwaje, huna budi kubatizwa tena upate kuwa Mbaptisti, kwa kuwa ni wa kukuingiza katika ushirika. Unaona?

22 Na sasa . . . Ndipo niliona nilipotaja jambo hili, kuhusu Malaika wa Bwana, kwa ndugu zangu, vema, walidhani nilikuwa nimerukwa na akili. Lakini, nikasema, "Ikiwa Mungu amenituma kufanya hivyo, kuna mtu wa kulipokea."

23 Ndipo nilipokuja miongoni mwa Wapentekoste, ilikuwa ni kama kuvaa glavu juu ya mkono baridi. Mnaona? Ilienea vizuri kabisa. Ndipo nilipokuja kujua walikuwa wamegawanyika katika madhehebu, wakizozana wenyewe kwa wenyewe, ni—nisingejiunga na lolote lao. Lakini, nilisimama moja kwa moja kwenye pengo, na kusema, "Sisi ni ndugu." Mnaona? "Sisi ni ndugu, hatupaswi kuzozana." Vema, maadamu tunazozana sisi kwa sisi, ibilisi anakaa kitako akicheka, ametushika. Hebu tuweke mabega yetu na juhudi pamoja, kama *Twendeni Askari Wakristo*, madhehebu yote yakisimama pamoja kwa jambo moja: Neno la Mungu. Jambo ndilo hilo. Chini ya Damu ya Mwanawe, Kristo Yesu, acha hiyo bendera ipeperuke.

24 Najua jana usiku, na nyakati mbalimbali, nimejaribu kuweka hizi jumbe rahisi tu niwezavyo, na kuwafanya waone, na kama wataamini tu ujumbe huo mdogo rahisi, Mungu atawaongoza.

25 Na—nami napata baadhi, mimi . . . Watu hufikiri ninasisimkwa ninapoanza kuhubiri, lakini sijasisimkwa, najua mahali hasa ninaposimama, lakini najisikia vizuri tu.

Na kwa hivyo, jamaa fulani anasema, "Una kichaa."

Vema, endapo ninacho, niacheni tu, ninajisikia vizuri zaidi hivyo kuliko ninavyojisikia vinginevyo. Kwa hivyo, i—inanikumbusha tu . . .

Baadhi yao wanasema, "Vema, sisi ni kanisa la kale, tulikuwa wa kwanza. Sisi . . . " Naam.

26 Nina hadithi ndogo, wakati mmoja, kuhusu watoto wangu. Mimi ni baba, nami na—nawapenda watoto wangu. Billy, mwanangu, mama yake alikufa alipokuwa tu jamaa mdogo, nami nimekuwa baba na mama pia kwake. Ningembeba kote, huku akimlilia mama, hakuna mama wa kumpa. Na hiyo ilikuwa ni kwa miaka kadhaa hadi alipokuwa mkubwa vya kutosha, kwenda shuleni. Nami, huko nje mikutanoni, nisingeweza kumtunza, kwa hiyo nikaoa tena, nasi tumekuwa na watoto watatu.

27 Nina wasichana wawili wadogo na mvulana. Rebekah, miaka michache iliyopita . . . yeye ndiye mkubwa zaidi, kidogo yeye ni mwembamba, miguu mirefu. Na—naye Sarah akaja, yeye kidogo ni mfupi. Naye Becky ana nywele nyeupe na Sarah ana nywele nyeusi. Becky ana macho makubwa ya bluu na nywele nyeupe, naye Sarah, zaidi sana kama mama yake, kidogo yuna nywele nyeusi na macho meusi. Na kwa hivyo, wote wawili ni wasichana wa baba hata hivyo.

28 Kwa hiyo basi, wao huningojea, bado, ninapoingia. Basi nilikuwa nje mikutanoni, nami nilikuwa nimechoka sana, lakini walikuwa wakingojea. Kila ndege iliyopita juu, wangesema, "Baba anakuja sasa!" Lakini, wakati ukaenda sana, baada ya kitambo kidogo, walikuwa na . . . mwana-mchanga akaingia machoni mwao, mwajua, kwa hiyo Mama akawalaza kitandani. Akangoja, nayo ndege ikachelewa. Nikaingia yapata saa saba usiku. Baada ya kutoka mikutanoni namna hii, mimi huchoka sana hata siwezi kulala.

Na kwa hiyo, nilikuwa nikimwambia Billy, nikija . . . Akasema, "Baba, unaonekana umechoka sana."

Nikasema, "Lakini Billy, lazima nitie kila juhudi."

29 Akasema, "Kwa nini usiende huko na kamwe usiongee na watu. Nawe useme tu, 'Nitawaombea wagonjwa,' na kufanyiza mstari wa maombi kama ulivyowaahidi na usihubiri."

Nikasema, "Billy . . . "

Akasema, "Hakuna watu wengi pale, baba, mkutano mdogo."

30 Nikasema, "Ningeweka juhudi zile zile huko endapo kuna laki moja." Mnaona? Nikasema, "Kwa sababu nimefungwa na upendo wa Mungu unaonibidiisha kwa Kanisa Lake." Mnaona?

31 Na mara nyingi nimewazia yale ningefanya na matone mawili ya Damu halisi ya Yesu Kristo, katika bilauri. Kile . . . Jinsi ningeishikilia! Bila shaka nisingeninii . . . nisingetaka kuimwaga. Ningeishikilia kifuani mwangu, na hadi moyoni mwangu, na kusema, "Bwana Mungu, jinsi ninavyoithamini Damu hii!" Lakini, machoni Pake, nina kikubwa zaidi alasiri ya

leo: ninacho kile kilichonunuliwa kwa Damu Yake mbele yangu. Aliwapenda kuliko alivyoyapenda maisha Yake Mwenyewe.

32 Basi inanipasa kuwatendeaje? Mwaminifu, mnyofu. Nayo dhambi sina budi kuikemea, haijalishi ni kiasi gani inakuumiza wewe au mimi. Sina budi kufanya kila niwezalo kuwa mwaminifu na mnyoofu, na mtumishi wa Kristo.

33 Tuirudie hadithi yangu. Hao wasichana wadogo, iliwabidi. . .Nisingeweza kulala, kwa hiyo nikaamka tu, nikaingia sebuleni, na kuketi kitini. Basi karibu mapambazuko nikasikia huko chini, chumba cha watoto, kitanda kikageuka kidogo, na Becky akaamka. Akaangalia nje, akaona kulikuwa kumepambazuka; kifuniko kikaondolewa, kisha akashuka ukumbini akaja upesi sana, akaniona nimeketi pale. Ndipo mtoto Sarah akaamka wakati Becky alipoamka. Basi Sarah alikuwa ni jamaa mdogo wakati huo, yapata umri wa miaka minne; naye Becky alikuwa na umri wa miaka minane, tisa.

34 Kwa hiyo, Sarah. . .Watoto wetu wanavaa nguo za kuachiwa. Mnajua, moja kutoka. . .aliye mkubwa zaidi anapata kitu, kisha kinaendelea chini katika familia. Kwa hiyo, Sarah alikuwa amevaa pajama ya Becky; na zile zenye mguu wa sungura—pajama za miguu ya sungura, kubwa, nao huo mguu mdogo sana wa Sarah katika pajama ya miguu mikubwa ya Becky. Na kwa hiyo, asingeweza kuendana naye, huku miguu hiyo mikubwa ya sungura ikipepesuka, mwajua.

35 Basi Becky akamtangulia Sarah kunifikia. Na kwa hivyo, akaruka juu ya mapaja yangu, akatupa mikono yote miwili shingoni mwangu, na kuanza kupaza sauti, "Baba!" Bila shaka, hiyo hufanya moyo wako kufurahia. Halafu akageuka, naye Sarah alikuwa akikaribia tu, hayo macho madogo meusi yakija, mwajua, kwa nguvu tu alivyoweza. Basi akaona Becky alikuwa amemtangulia, ndipo maskini jamaa huyo mdogo, alionekana tu amevunjika moyo sana.

36 Kwa hiyo, akaangalia pande zote. . .Becky akaangalia pande zote, akasema, "Sarah, dada yangu, nataka ujue jambo fulani." Akasema, "Nilikuwa hapa kwanza." Hivyo ndivyo kanisa kubwa linavyojaribu kutwambia. "Nilikuwa hapa kwanza, na ninaye Baba wote, wala hakuna aliyesalia kwako."

37 Loo, jamani! Maskini Sarah, ilimwumiza sana, mwajua. Midomo yake midogo ikaanza kutetemeka, macho yake makubwa meusi yakabadilika kidogo, akaanza kugeuka, nami nikamwelekezea kidole changu, namna *hiyo*, na kuuchomoa mguu wangu. Kwa hivyo, huyu hapa anakuja, macho yake yakaangaza, naye akaja na kutagaa mguuni mwangu, lakini kidogo alikuwa Shaghalabaghala, kama tusemavyo huko chini. Yeye. . .ninii yake. . .hakuwa amekaa hapa muda mrefu sana, kama lile kanisa changa, mwajua, kidogo alikuwa hajatulia.

Na kwa hiyo, nami, ili kumzuia asianguke, nilimkumbatia kwa mikono yangu na kumvuta karibu nami.

38 Akalala hapo kidogo, kisha akageuza kichwa chake kidogo, akamtazama dada yake, akasema, "Rebekah, dada yangu," kasema, "huenda ikawa kweli kwamba unaye Baba wote, lakini nataka ujue jambo moja: Baba yuna mimi wote!"

39 Kwa hiyo—kwa hiyo hivyo ndivyo ninavyohisi kuhusu hilo. Huenda nisiwe na elimu, sifa, kama mhudumu anavyopaswa kuwa nazo, lakini jambo moja nijualo, kidogo ninaweza kuwa shaghalabaghala, lakini nataka Yeye awe na mimi wote. Mradi tu anashikilia, hilo linanitosha mimi.

40 Na sasa, asanteni kwa usaidizi wenu mzuri. Kunachelewa, sasa, najua mna ibada zenu usiku wa leo. Mungu awabariki. Na sasa, ikiwa ninaweza kuwa na fadhila kwenu, niandikieni. Sijaribu kupata anwani yenu. La. Mara nyingi, huo ni ukogo wa kujitangaza ambao . . . Ha—hata sininii . . . Nina katibu mmoja, na dawati moja dogo lililowekwa pembeni mwa trela. Na hivyo ndivyo tunavyojaribu kujibu barua. Lakini, ni kule kuwazia, iwapo tunaweza kuwasaidia. Msininii . . . Kitambaa cha maombi, nitafurahia kukutumia kimoja, ama chochote niwezacho. Hakuna malipo, hakuna malipo kwa chochote.

41 Na, mara nyingi tunajua, kasema, "Niandikieni." Halafu basi, muda si muda mwajua, unaendelea kujenga, kujenga. Mnajua jinsi ilivyo, kwa sababu watu hawana budi kupata usaidizi huo wa watu ili kuendeleza vipindi vya televisheni na ujumbe wa redio. Sina chochote cha mambo hayo. Sihitaji pesa. Ni—ningeninii . . .

42 Sasa, mtu kama Ndugu yetu mwenye fadhili Oral Roberts angewezaje kuja kwenye mkutano kama huu wakati inambidi kuwa na karibu dola elfu kumi hadi kumi na tano kila siku? Angewezaje kufanya hivyo? Asingeweza. Ni hayo tu. Asingeweza kufanya hivyo.

43 Kwa hiyo, basi, nafikiri Bwana, Yeye kamwe, Yeye—Yeye—Yeye ni mwerevu, Naye ni hekima yote, sina akili ya kutosha kufanya hivyo, kwa hiyo nakaa tu, nataka kudumu tu "Ndugu Bill," na kuendelea popote aniongozapo. Ikiwa ni mahali padogo, ambapo hakuna kitu, mbona, ninaenda huko.

44 Na kama . . . Aliniongoza kwenda Afrika, nilienda huko kwa ajili ya watu laki mbili au tatu, nikaenda India, laki tano, lakini kwa namna fulani, mtu fulani anakuja tu na kuulipia, nasi hao tunaondoka. Kwa hiyo, ninaishi tu kwa imani, hivyo tu. Na kwa hiyo, ninaweza kwenda popote anaponiita, haijalishi ni wapi, ninaweza kwenda. Mnaona? Kwa kuwa . . . ninayo . . . Vema, kama ingenibidi kufadhaika juu ya kukusanya dola elfu kumi na tano, ishirini na tano kwa siku, whiu, jamani, ningekuwa na upara mkubwa kuliko nilio nao sasa.

45 Nikizungumza juu ya kuwa mwenye upara, utani mdogo kwa mke wangu, hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikizichana nywele hizo mbili ama tatu, mwajua.

Naye akasema, "Billy, unakaribia kuingia upara mtupu."

Nikasema, "Lakini, sijapoteza hata mmoja."

Akasema, "Naomba, niambie zilipo."

46 Nikasema, "Vema, mpenzi, nitakwambia, utakaponiambia mahali zilipokuwa kabla sijazipata; popote zilipokuwa basi, zinaningojea niziendee." Kwa maana Biblia ilisema, "Msijali, nywele za vichwa vyetu zilihesabiwa, Angefufua kila kitu, hakuna kilichopotea."

47 Ninamwamini Mungu ambaye atatuinua katika siku za mwisho. Naam, bwana. Loo, jinsi ningependa kuzungumza nanyi juu ya hilo kwa muda kidogo alasiri ya leo. Elekeza tu imani yako kwenye ufufuo huo, na uone hiyo picha kuu iliyowekwa mle ndani, jinsi ilivyo nzuri, jinsi wazee wanavyobadilika wakawa vijana, na—na jinsi Mungu alivyotoa ahadi, na kuithibitisha kupitia kwa Sara na Ibrahimu, kuwarudisha wote wawili kuwa kijana mwanamume na mwanamke. Na kuonyesha yale atakayowafanyia Uzao wao wote baada yao. Na kwa hiyo, yote ni mazuri!

48 Na moja ya siku hizi, Mungu akipenda, na ikiwa hamjali, na mtaninii. . .na—na mtaniruhusu kurudi, ningependa kurudi humu kisiwani, nipige hema mahali fulani, na kukaa majuma manne ama matano ama chochote kile, ili tupate tu kuwa na wakati mwingi. Hivyo basi. . .[Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Asanteni sana. Hiyo inanifanya nijisikie kukaribishwa sana. Na mimi—mimi ningefanya chochote. . .

49 Mnaona, watu wengi hawaelewi uponyaji wa Kiungu ipasavyo, nami naweza kuwa papa hapa. Lakini nikipita hivi, na muda si muda mwajua, wasioamini wanawazunguka waaminio, na kujaribu kulifafanua vinginevyo, na, mwajua. Basi—basi jambo la kwanza mwajua, ugonjwa unamshika mtu, hawajui tu. . .ni baada ya kuombewa, nao wanawazia, "Loo, vema, nimepoteza uponyaji wangu." Wakati mwingine hiyo ndiyo ishara hasa kuwa umeupata. Unaona? Nawe. . .Nao hawajui jinsi ya kuishikilia. Na kama tungeweza tu kuketi chini na, ugonjwa ukirudi tena ama jambo fulani, ungeweza kurudi. Tungeweza kuketi mbele za Bwana katika mahali maalum, ambapo kila mtu binafsi, tungeweza kuona kile kinachotokea.

50 Maono haya yanayotokea hapa, mnafanya hivyo ninyi wenyewe, hayo ni maono madogo tu ya muda, kama vile unamgusa, bali maono halisi ni wakati Mungu anapoonyesha kitakachokuwa, na kile kimekuwa, kile kijacho, na kadhalika namna hiyo.

51 Sasa, Bwana daima awabariki na kuwapa afya na furaha. Na mniombee sasa. Na tuinamishe vichwa vyetu huku tukiomba baraka za Mungu. Ninakusudia alasiri ya leo kuwaombea wagonjwa wote katika mstari utakaopita. Je, una haja ambazo ungependa zijulikane kwa kuinua mkono wako? Asanteni, na Mungu awabariki.

52 Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru sana kwa ushirika na wakati ambao tumekuwa nao pamoja katika kusanyiko hili la kupendeza pamoja na Kanisa la Mungu aliye hai, wale waliotoka madhehebu mbalimbali na matabaka ya maisha wamekusanyika pamoja kukuabudu Wewe tena alasiri ya leo. Tunashukuru kwa ajili ya jambo hili, kwa Imani iliyokabidhiwa mara moja kwa watakatifu, iweze kurejeshwa tena katika siku za mwisho, kwa kuwa imetabiriwa hivyo.

53 Tunaomba baraka Zako juu ya kila haja. Mungu, wabariki watu hawa. Na jalia magonjwa yawaondokee kabisa. Jalia wachungaji wasikie kusanyiko lao likitoa ushuhuda majuma kadhaa tangu sasa, kwamba ma—matatizo ya tumbo, na maumivu, na magonjwa waliyokuwa nayo, yamepita, hawanayo tena. Jinsi tutakavyoshukuru kwa jambo hilo, Bwana, Nawe sikuzote umelitenda. Nami najua Wewe huna upendeleo wa mahali au mtu, utatenda tena.

54 Utubariki sasa. Na tunapolikaribia Neno Lako, jalia Roho Mtakatifu atufunulie mambo yaliyoandikwa humo. Na utupe imani kwa ajili ya mkutano ujao, Bwana, mstari wa maombi unaokaribia kufanywa katika dakika chache zijazo. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

55 Sasa, mkipenda, fungueni pamoja nami kwenye ujumbe mdogo mfupi tu. Nami ningetaka kuwahubiria alasiri ya leo, lakini mimi. . .nimepwelewa na sauti kwelikweli kooni mwangu. Na ningefurahi kuweza kuzungumza baada ya mikutano hii yote, na upepo wa kila namna, na kila kitu kupitia mi—mijengoni.

56 Sasa, ninawatakeni mfungue Injili ya Mathayo Mtakatifu mlango wa 15 na kifungu cha 21 hadi cha 28. Ninataka kusoma sehemu yake kubwa hapa, nami nawatakeni mnifuate, mkiweza. Kifungu cha 21:

> *Yesu akaondoka huko, akaenda kando* pwani *za Tiro na Sidoni.*
>
> *. . .tazama, mwanamke Mkananayo wa* pwani zile *akatokea, akampazia sauti akisema, Unirehemu,. . . Bwana, mwana wa Daudi; binti yangu amepagawa sana na pepo.*
>
> *Wala yeye hakumjibu neno. Nao wanafunzi wake wakamwendea, wakamwomba, wakisema, Mwache aende zake; maana* anapiga kelele *nyuma yetu.*

*Akajibu, akasema, Sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.*

*Naye akaja akamsujudia, akisema, Bwana, unisaidie.*

*Akajibu, akasema, Si vema kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.*

*. . . akasema, Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula . . . makombo yaangukayo mezani pa bwana zao.*

*Ndipo Yesu akajibu, akamwambia, Mama, imani yako ni kubwa: na iwe kwako kama utakavyo. Akapona binti yake tangu saa ile.*

57 Ningependa kuchukua so—somo kutoka kwa hili, nitatumia neno moja, na neno hilo ni: *Anayeng'ang'ania.* Nalo neno *anayeng'ang'ania* maana yake ni "kuwa mwenye kushikilia." Webster inasema kwamba ni "mwenye kushikilia kwa dhati katika kutimiza lengo." Kujaribu kufanya jambo, na kulishikilia kwa dhati, unakuwa mwenye kung'ang'ania.

Watu wa nyakati zote, ambao wana imani katika yale wanayojaribu kufanikisha, wamekuwa wa kung'ang'ania. Huna budi kuwa na imani katika yale ufanyayo.

58 Nimeona, na limekuwa jambo zuri sana kupitia miaka thelathini katika—katika, miaka thelathini na mmoja, hasa, nyuma ya mimbara, na yapata miaka kumi na sita sasa ndani, kila mara kote ulimwenguni katika mistari ya maombi, na nikiwaangalia watu, watu sikuzote, kamwe hutaninii . . . ni kwa nadra unamwona mtu ambaye atakiri kwamba hawana imani, daima wana imani yote.

59 Lakini mnaona, imani ni tofauti na vile unavyowazia ndivyo, ama, si vile wewe, ninamaanisha jinsi mtu wa kawaida angewazia. Mara nyingi, ni tumaini badala ya imani. Una dhana ya kiakili ya imani, kile inachomaanisha, na kiakili unayo imani, lakini zama ndani zaidi ya hapo, unaona, zama ndani zaidi. Imani ina hakika, ni bayana. Ni, si hadithi ya kubuni, si ma—mawazo ya kiakili, lakini ni bayana, na bayana ni kitu ambacho unaweza kushikilia. Unaona? Ni "kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, na ni bayana ya mambo yasiyoonekana," katika, Waebrania, wa kwanza . . . mlango wa 11, kifungu cha kwanza. Sasa, kwamba imani siyo . . .

60 Sasa, una hisi tano mwilini mwako, Mungu alikupa hizo hisi tano kuwasiliana na makao yako ya duniani, hizo ni kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia. Lakini hizo hazina uhusiano wowote na Mungu, hakuna mojawapo itakayomtangaza Mungu, si hata mojawapo, hapana, kwa sababu umepewa tu hizo kuwasiliana na makao yako ya duniani. Unaona? Kuona, kuonja, kugusa, kunusa, kusikia. Unaona, hizo hazina uhusiano wowote na Mungu. Na watu *kweli* huzitegemea, lakini hu—hu—hupaswi kufanya hivyo.

61 Imani ni kitu tofauti, imani ni hisi ya sita, ambayo unawasiliana na Mungu. Unaweza tu kuwasiliana na Mungu kwa hisi ya sita, ambayo ni imani. "Yeye amjiaye Mungu hana budi kuamini kwamba yeye yuko, na huwapa thawabu wale wanaomtafuta kwa bidii." Unaona? Sasa, ni jambo la kipekee sana.

62 Sasa, kwa mfano hapa, sasa, nitazungumza kwa sauti kubwa, sasa, hii hapa ala ya muziki. Unajuaje kuwa ni a—ala ya muziki? Kwa sababu nina hisi moja ambayo itawasiliana nayo, hiyo ni macho yangu: Naiona hiyo ala; siisikii, siinusi, siigusi, siionji, lakini kuna hisi moja tu inayowasiliana nayo.

63 Sasa, mmeusikia ule usemi wa kale, "Ninatoka Missouri, huna budi kunionyesha." Mnaona? Loo, unaitwa "mkoa wa nionyeshe." Sasa, acha nikuonyeshe jinsi usemi huo ulivyo wa kimzaha. Sasa, haiwezekani kabisa kwangu kutumia hisi ya kuona kujua kwamba hiyo ala bado iko pale, mtu fulani angeweza kuwa amekuja na kuichukua kutoka nyuma yangu, haiwezekani. Siioni, iko nyuma yangu, bali ipo.

64 Sasa, kuona si kuamini, mnaona, kuona si kuamini, kwa sababu nina hisi nyingine, ambayo ni kugusa. Nako kugusa ni kuamini hapa, na ni halisi tu kama kuona, kwa sababu ni ala. Ninaigusa, shingo juu yake, nagusa kamba juu yake, nagusa vibao ambavyo vimezifunga hizo kamba. Mnaona? Na kwa hivyo, kuona sio kuamini. Ninaamini kuwa iko pale kama vile tu ningekuwa nikiiangalia. Mnaona ninachomaanisha?

65 Sasa, jambo lile lile kwa hisi nyingine yoyote. Sasa, watu wanaposema kwamba "kuona ni kuamini," ni dhihaka kwa tamshi lao wenyewe. Mnaona? Ni—ni—ni fedheha kwa akili zao, kuwazia kwamba kuona ni kuamini, hiyo inatupilia mbali hisi zingine zote.

66 Sasa, kwa mfano, tuseme kwamba hii ilikuwa chupa ya manukato, tuseme tu ilikuwa ni manukato. Vema. Sasa, na—naiona, na ninaigusa, bila shaka, kwa mikono yangu. Lakini, vipi kama sikuweza kuiona, wala singeweza kuigusa, na hata hivyo, mtu fulani angeitwaa, nami sikuiona wala sikuigusa, nayo ikasogezwa karibu nami, ningeweza kuwaambia ilikuwapo, kwa sababu hisi yangu ya kunusa inaingia kazini, mnaona, wakati hisi zangu zingine hazitaitangaza. Sasa, mnaelewa ninachomaanisha?

67 Sasa, "Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo" usiyoyaona, usiyoyaonja, usiyoyagusa, usiyoyanusa, wala kuyasikia. Mnaona? Kwa kweli ni hisi, kwamba unajua, hakuna kulikwepa, una hakika. Ndipo jambo fulani litatukia, ukiwa na hiyo.

68 Kama ambavyo nimesema mara nyingi: Vipi kama ningelikuwa nimesimama hapa kwenye mojawapo ya vilele hivi vya mlima nikifa kwa njaa, wala hakuna mtu angenipa

pesa zozote, na mkate u—ungeyaokoa maisha yangu, nawe uje na kunihurumia, ndipo unipe mkate, au, labda, tuseme unipe senti ishirini na tano? Tuseme—tuseme hiyo ndiyo bei ya mkate, ulinipa senti ishirini na tano. Vema, ninaweza kufurahia tu hizo senti ishirini na tano mkononi mwangu, kadiri ningeweza kufurahia nikiwa na mkate mkononi mwangu. Kwa nini? Nina uwezo wa kununua mkate. Jambo pekee ninalopaswa kufanya, ni kwenda kule, dukani, na kujinunulia mkate. Lakini sasa, sasa hivi, nina uwezo wa kununua mkate, unanunua mkate; hiyo ni imani.

69 Imani kamwe haiangalii na kusema, "Sijisikii vizuri zaidi; sioni vizuri zaidi; sisikii vizuri zaidi." Mnaona? Inafurahi, kwa sababu tayari umepata uwezo wa kununulia uponyaji wako. Unaona? Una furaha vivyo hivyo, sawasawa na . . . unajua vizuri kabisa kwamba tayari unao, kwa sababu una bei yake ya kuinunulia, ambayo ni imani. Unaona? Imani hailegei kamwe.

70 Vema, nitarudi kwenye somo langu. Vema. Lakini, niliwazia ningeingiza hilo ili mweze kuona ina kilindi zaidi kuliko yale ambayo watu wanasema kijuu juu, "Loo, ni—ninaamini." Unaamini kiakili, lakini ikiwa kweli unaamini, kila kitu katika Biblia hii ni chako. Unaona? Ni imani yako, inunue. Unaona? Hizi hapa bidhaa, zimewekwa tu hapa, Mungu, Mwenyewe, katika umbo la herufi, na imani katika Neno hilo hukununulia kitu hicho, hukifanya kutimia, hukifanya kiishi.

71 Sasa, nilikuwa kwenye ninii . . . Nilizungumza katika Klabu ya Kiwanis wakati fulani uliopita, na kulikuwa na daktari aliyeniambia kwamba, akasema, "Loo, ninaamini, Billy. Mimi . . . " Nilikuwa nikizungumza juu ya mgonjwa fulani ambaye alikuwa amemkatia tamaa, naye Bwana akamponya. Akasema, "Loo, na—naamini katika imani, imani."

Kisha nikasema, "Sasa, ngoja kidogo. Unazungumzia imani ya aina gani?"

72 Akasema, "Imani tu." Kasema, "Ninaamini kama mtu huyo angetoka hapa, na kuweka mkono wake juu ya mti, na kuamini kwamba angepona, angepona vile vile tu, sawasawa na vile mtu fulani angalimwombea."

73 Nikasema, "Sasa, ni nani . . . niambie, daktari, wewe ni mtu anayeonekana kuwa na akili, mtu angewezaje kuwa na imani kwamba 'kuweka mkono wake juu ya mti kungemponya'? Huna budi kuwa na imani katika kitu fulani, na Biblia ilisema, 'Imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu.' Huo ndio msingi wake, imani yako ina msingi, kwa maana Mungu aliahidi jambo hilo."

74 Kama vile Ibrahimu, mbona, alipokuwa . . . mkewe alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano naye alikuwa na sabini na mitano, mbona, walikuwa wameishi pamoja, yeye . . . walifunga ndoa alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, kumi na saba,

alikuwa amemzidi umri kwa miaka kumi, alikuwa dada yake wa kambo. Na baada ya kuishi kama mume na mke miaka hii yote, hebu tuone, sitini na mitano, alikuwa amekoma hedhi kwa miaka kumi, kumi na mitano.

75 Sasa, huyu hapa Ibrahimu, umri wa miaka sabini na mitano, mzee, ndipo Mungu akamtokea, na kusema, watampata mtoto. Mbona, jamani, hilo kwa Ibrahimu lilikuwa ni sawa na kumpata huyo mtoto mchanga, tayari alikuwa naye, kuhusiana na hilo.

76 Inaweza . . . Vema sasa, wakati mwingine imani itakufanya utende kigeni kwa ulimwengu. Sasa, mngeweza kuwazia mume na mke wakongwe hivyo wakishuka, wakiandaa nafasi hospitalini? Wangesema, “Afadhali umfungie huyo mzee, ana kasoro, anahitaji kumwona daktari wa akili au kitu fulani.”

77 Lakini, Ibrahimu alikuwa na imani katika kile ambacho Mungu alikuwa akisema. Sasa, siku za kwanza zikapita, ule wakati wa kawaida wa siku ishirini na nane. Ninaweza kumwona akimwendea Sara na kusema, “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hakuna tofauti hata kidogo.”

78 “Mbona, utukufu kwa Mungu, tutampata kwa vyovyote vile.” Unaona? “Tayarisha buti zote, na pini, na jicho ndege, andaa kila kitu, kwa sababu tutampata mtoto.”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo, hilo latosha.” Miaka kumi ikapita. “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

79 “Utukufu kwa Mungu. Ni miaka-kumi-zaidi ya mwujiza kuliko vile ingekuwa huko nyuma. Itatendeka kwa vyovyote vile.” Miaka ishirini na mitano ikapita. Sasa yeye ana mia moja, naye mke tisini. “Unajisikiaje, mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Utukufu kwa Mungu. Tutampata kwa vyovyote vile. Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Mungu alisema hivyo.” Sasa mnaona?

80 Nayo Biblia ilisema, “Ibrahimu hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu.” Sasa, sisi, kama tukiwa ndani ya Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu, nasi tu warithi pamoja naye sawasawa na ahadi. Hiyo ni kweli? Basi Mzao wa kweli wa Ibrahimu angewezaje kuona ahadi ya Mungu hapa, halafu alalamikie kuumwa na tumbo, ama mkono wako haujanyooshwa sawasawa, bado, wakati Mungu alitoa ahadi? Amina. Kama ukisubiri miaka hamsini, inaleta tofauti gani? Ibrahimu aliweza kufikia cheo cha baba wa mataifa na kumpata mtoto, kwa sababu aliamini naye alikuwa aking’ang’ania kwa imani yake. Mbona, angeweza kung’ang’ania, Mungu alikuwa ameahidi! Naye Mungu ni . . .

Alishawishika, kikamilifu, ya kwamba Mungu alikuwa na uwezo wa kufanya kile alichokuwa amesema. Loo, jamani! Hmm!

81 Uzao wa Ibrahimu unawezaje, Uzao wa Kifalme wa Ibrahimu, Kanisa la Mungu aliye hai, kuangalia ahadi, halafu wasiiamini? Neno la milele la Mungu, "Mimi ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi." Mnaona? "Mkikaa ndani Yangu, nalo Neno Langu likae ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtapewa." Mnaona? Loo, ni ahadi za namna gani anazotupa! Tungeweza kuzinukuu. Lakini, u—unaweza tu kung'ang'ania unapolishika Neno.

82 Sasa, kama mtu fulani akija, akasema, "Utukufu kwa Mungu, jisikie hivi. Haleluya! Ninalo mikononi mwangu." Sasa, nisingeweza kung'ang'ania hilo sana, mnaona, kwa sababu hakuna mtu anayeweza kukuponya: Hakuna dawa, hakuna daktari, hakuna kitu kilichowahi kumponya mtu yeyote, ila Mungu.

83 Nataka unionyeshe daktari anayedai kuwa yeye ni mponyaji. Nataka uniandikie maagizo ya dawa ambayo yatafanya chochote kuelekea uponyaji. Mayo ndio bora zaidi tulio nao, nimehojiwa huko mara mbili. Walisema, "Hatudai kuwa waponyaji, Bw. Branham, tunadai tu kuyasaidia maumbile, Mungu ndiye Mponyaji."

84 Wanaweza kukata mahali, lakini inahitaji uumbaji kujenga tishu kupaponya tena. Wao. . . Sasa, mnasema, je, unawahukumu madaktari? La hasha. Kama ukivunja mkono wako, daktari amejifunza jinsi ya kuuweka vizuri mkono huo, lakini hawezi kuuponya. Mungu hana budi kuuponya, Hana budi kutoa kalisi na yote yanayoingia kwenye huo mfupa, na kuushona huo pamoja, na kuuponya. Anauweka tu vizuri.

Kama uliuvunja mkono wako, kisha ukamwendea daktari, na kusema, "Uponye, daktari, nataka kumaliza kuosha vyombo vyangu."

Angesema, "Unahitaji uponyaji wa akili." Hiyo itakuwa ni karibu sawa. Unaona? Lakini u—unapaswa. . . Daktari anauweka vizuri, lakini Mungu ndiye Mponyaji.

85 Huwezi kulifanya Neno la Mungu liseme uongo. Alisema, "Mimi ni Bwana Mungu wako, niponyaye magonjwa yako yote." Wala hawajawahi kupata dawa ambayo ingeponya. Hakuna daktari anayedai kuwa inaponya. Inaua tu vijidudu huku Mungu akiponya. Inasafisha tu kidonda, au—au kitu kama hicho.

86 Au, anaushika mkono wako, daktari hufanya kazi kwa hisia mbili, anachoweza kugusa kwa mikono yake au kuona kwa macho yake, anaweza kuugusa uvimbe, aseme, "Naam, una uvimbe hapo, nitaukata." Sasa, yeye hutoboa shimo hapo, na kuukata. Sasa, hakuuponya, aliukata huo uvimbe. Nani huponya? Anashona, lakini iwapo Mungu hata—iwapo Mungu hatauponya, utakuwa hivyo daima, mnaona, utakuwa hivyo

daima. Anaweza kung'oa jino, lakini ni nani atakayeponya mahali lilipotoka? Anaweza kuuweka mkono vizuri, lakini ni nani atakayeuponya? Mungu ndiye Mponyaji.

87 Kwa hiyo, unaona, ukiliweka Neno la Mungu ndani yako, pamoja na imani ya kuamini Neno hilo, jambo fulani litatukia, na hutaliacha kamwe. Kweli.

88 Nawazia juu ya baba wa taifa letu ambaye. . .ambaye anaitwa George Washington. Sikuzote nilimheshimu sana Bw. Washington kwa sababu alikuwa Mkristo.

89 Na mbele ya Bonde la Forge, wakati alipoomba usiku kucha kwenye theluji, mpaka akalowa hata kiunoni mwake, na askari wake, theluthi mbili yao hata hawakuvaa viatu, walikuwa wamefunga miguu yao kwa kitu chochote walichoweza kuifungia, na hali ya hewa ilikuwa sifuri, nao huo mto umeganda, usiku huo aliomba mpaka akalowa hadi kiunoni mwake, akapata ono kutoka kwa Mungu, ndipo kesho yake, akang'ang'ania sana. Alivuka huo mto bila kujali . . . Makorongo ya barafu hayakumzuia. Kisha risasi tatu za gobori zilipigwa zikapitia kotini mwake, naye akaendelea hata akapata ushindi. Kwa nini? Aling'ang'ania. Aliomba mpaka akamshika Mungu, na kujua kile Mungu alikuwa amesema. Hivyo ndivyo. Angeweza kung'ang'ania apate mafanikio.

90 Na jambo la kwanza, mafanikio yako ni kwa njia ya nia yako na lengo lako tu. Nia yako haina budi kuwa sahihi na lengo lako halina budi kuwa sahihi. Ikiwa lengo lako ni sahihi, na nia yako ni mbaya, basi halitatendeka. Inakubidi kuwa na lengo sahihi na lazima uwe na nia sahihi. Na kisha ulichukue kwa uongozi wa Roho Mtakatifu moyoni mwako na ukae nalo, Mungu atalitimiza.

91 Nuhu, mtu mashuhuri wa Mungu, aling'ang'ania sana katika siku zake. Aliishi katika wakati wenye akili kuliko wakati tunaoishi, wakati wa kisayansi kuliko wakati tunaoishi, kwa sababu katika siku hizo walijenga piramidi, tusingeweza kuijenga.

92 Nimekuwa Misri kwenye zile piramidi. Sfiniksi, tusingeweza kuzijenga tena hata tufanyeje. Baadhi yao . . . Na piramidi hiyo imewekwa kikamilifu kijiografia katikati ya dunia, mpaka hakuna kivuli kuizunguka, haidhuru jua liko wapi. Mnaona? Na jambo lingine, kuna majabali mle ndani, juu kabisa hewani, ambayo, hatuna mitambo, hakuna nguvu za petroli ambazo zingeweza kuyanyanyua majabali hayo huko juu. Mnaona? Lakini, waliijenga. Wangeweza kuifanikisha. Walikuwa na nji— njia ya kufanya hivyo, labda nguvu za atomiki, nguvu za haidrojeni, kitu fulani. Lakini, nguvu za petroli na nguvu za umeme, usingeweza kutengeneza mtambo mkubwa vya kutosha kuyanyanyua huko juu. Kwa hiyo, waliyapandishaje huko? Na ni uashi mkamilifu sana, hata huwezi kuingiza wembe ma—mahali

ambapo yameumana, na mamia na mamia ya tani. Walifanyaje jambo hilo? Walizijengaje?

93 Wangeweza kutengeneza mumiani, kuchukua mwili na kuupaka dawa usioze hata ungali na sura nzuri hata wa leo, baada ya karibu, karibu miaka elfu nne iliyopita, bado unaonekana wa kawaida, rangi ambayo hatuwezi kufanyiza tena kamwe. Walikuwa werevu, wenye akili. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

94 Je, wajua akili na werevu ni alama ya dhambi na uharibifu? Fuata ukoo wa—wa watoto wa Hamu. Waangalie watoto wa Kaini: Wote wanakuwa, hata kufikia wakati uliotangulia gharika, walikuwa watu werevu, stadi, wenye akili, nao walikuwa wanasayansi, wao, wajenzi wa chuma, na kadhalika. Lakini, watoto wa Sethi walikuwa wakulima wanyenyekevu, waliozaa Henoko na Nuhu. Lakini, hawa wengine walikuwa watu wa kisayansi, wenye elimu, werevu, wajanja.

95 Je, Yesu hakusema watoto wa usiku wana akili kuliko watoto wa mchana? Aliwafananisha watu Wake na wana-kondoo. Kuna mtu yeyote aliyewahi kuchunga kondoo? Mwana-kondoo, anapopotea, amepotea kabisa; hawezi kupata njia yake hata kidogo. Hana budi kuwa na kiongozi. Na hivyo ndivyo tulivyo, hatutakiwi kujua mengi sana, ya kutosha tu kumwishia Mungu; naye Mungu ndiye Kiongozi wetu anayetuongoza, lakini hatumruhusu kufanya hivyo, tunarudi nyuma kama mbuzi na—na kufanya yasiyofaa. Mnaona? Lakini, sisi . . . ni . . . Hizo—hizo ni alama zao.

96 Na katika siku za Nuhu, wakati Nuhu alipojitokeza na kusema, "Mvua itanyesha," alihubiri miaka mia moja na ishirini kwamba maji yatamwagika kutoka angani. Hakukuwa kumewahi kuwa na maji yoyote huko juu, la bwana, hakukupata kuwa na maji angani. Je, ungeweza kuwawazia hao wanasayansi wa siku hizo? Hiyo haikutosheleza vipimo vyao vya kisayansi. Wala Roho Mtakatifu siku hizi hatoshelezi vipimo vya kisayansi. Wala miujiza na ishara za Mungu hazitoshelezi vipimo vyao vya kisaya- . . . wanachofikiri kinapaswa kuwa sawa, vipimo, nilitaka kusema, lakini haileti tofauti yoyote, Mungu alilinena, na liko hivyo kwa vyovyote vile. Na imani inayoweza kulishika, hulishikilia.

97 Angalieni, Nuhu. Ningeweza kumwona mwanasayansi mkubwa akijitokeza na kusema, "Mnajua, kuna mzee huko juu ya kilima anayekijenga kitu cha namna fulani, kitu kama ghala kubwa mno huko juu ya kilima, asema, 'Mvua itanyesha, itakifanya kielee, maji yatashuka kutoka angani.'"

98 Anakwenda huko, kasema, "Nuhu, ngoja nikuonyeshe kuwa wewe ni . . . una udanganyifu wa kiakili, una kasoro. Ninaweza kuchukua chombo changu hapa na kukirusha mwezini, naweza

kuchukua rada yangu," vitu walivyokuwa navyo siku hizo, maana Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu," "wala hakuna maji huko juu. Sahau, ewe mzee, rudi shambani mwako, sahau hilo, hakuna maji huko juu, unatwanga-twanga bure."

Lakini Nuhu akasema, "Mungu alisema itanyesha."

"Naam, Mungu atapata wapi," sasa sikilizeni, "chochote huko juu, wakati hakuna kitu huko juu cha kuileta?"

Akasema, "Kama Mungu alisema kutakuwa na mvua, Yeye anaweza kuiweka mvua kule, kwa sababu Mungu alisema hivyo."

99 Haikumzuia hata kidogo, aling'ang'ania. Aliendelea moja kwa moja kujenga, kitu hicho, kwa sababu, kukiweka kitu hicho pamoja, kwa sababu aling'ang'ania, kwa sababu alijua ya kwamba Mungu alisema hivyo, na mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Lake haliwezi. Atafanya mafanikio Yake kuwaokoa wale waliotaka kuokolewa. Hakika.

100 Musa, mbona, yeye alikuwa mwanasayansi. Jamii ya Wamisri ilikuwa ndiyo watu werevu kuliko wote ulimwenguni mwote katika siku hizo, lakini Musa hata angeweza kuwafundisha Wamisri hekima. Naye alijaribu mbinu zake za kijeshi kuwakomboa wana wa Israeli, haingefanikiwa, akatoroka. Wakati mbinu zake za sayansi ya kijeshi zisingefanya kazi, Musa alikimbia kutoka mbele ya watu ambao Mungu alikuwa amemtuma kuwakomboa.

101 Wakati mmoja, upande wa nyuma ya jangwa, kichaka kilikuwa kikiwaka moto, naye Musa akasimama aone kilikuwa ni nini, ndipo Sauti ikatoka pale na kusema, "Vua viatu vyako, Musa, kwa maana ma-. . .mahali unaposimama ni nchi takatifu." Ndipo Musa akaenda mbele za Bwana, naye Bwana akanukuu Maandiko, "Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, nami ninakumbuka. . .ahadi Yangu kwa Ibrahimu, nao wakati umekaribia, nami nasikia kilio chao huko Misri, na nimeshuka. Ninakutuma huko chini kuwakomboa."

102 Mungu daima hufanya kazi kupitia wakala: mwanadamu. Mwanadamu ni wakala wa Mungu sikuzote, si kanuni za imani, si madhehebu, bali mwanadamu. Unaona? Mungu hakuwahi kufanya kazi kwa mitambo wala hajawahi kufanya kazi kupitia madhehebu, yanakufa mara tu yanapoundwa, hilo latosha milele. Niambieni, nataka mwanahistoria asimame, na kuniambia mahali ambapo kanisa liliwahi kujiundia madhehebu ambalo halikuingia mavumbini, sikuzote. Hiyo ni kweli kabisa. Kila moja yao, Yeye huyaweka kwenye rafu, kila moja yao ni mazao ya kanisa Katoliki, lile dhehebu la kwanza.

103 Marehemu papa, papa sasa hivi, huyu John XXII ndiye, nafikiri wanamwita, alitoa tangazo, nadhani magazeti yenu ya

Canada yaliliandika, kasema, "Makanisa yote: Rudini mahali Kanisa lilipoanzia, kule Rumi."

104 Ninataka mtu yeyote, mwanahistoria yeyote, anionyeshe ambapo Kanisa lilipoanzia Rumi. Madhehebu yalianzia Rumi, lakini Kanisa lilianzia Yerusalemu siku ya Pentekoste, ndipo Kanisa lilipoanzia. Ikiwa mnataka kurudi mwanzoni, niko tayari kurudi na papa, hadi mwanzoni, hiyo ni kweli kabisa, mkitaka kurudi pale Kanisa lilipoanzia.

105 Lakini sasa, madhehebu, Kanisa Katoliki ya Kirumi, ndilo kanisa la kwanza kuunda dhehebu ulimwenguni, nalo ndilo mama wa hayo yote. Pia Ufunuo 17 ilisema lilikuwa kahaba, na binti zake walikuwa makahaba, malaya, na wote wanapaswa kuangamizwa, hiyo ni kweli kabisa. Sasa, hilo ni Neno la Bwana, naam, wewe bishana Naye, unaona, si mimi, maana ninanukuu tu aliyosema. Angalieni, hiyo ni kweli. Na kisha tunavikumbatia vitu hivyo, na, mbona, ni la kuchukiza sana.

106 Musa, alipopata ono hilo kutoka kwa Mungu, naye Bwana akamtokea, Naye akamnukulia Neno Lake la ahadi, Musa alikuwa njiani akienda zake moja kwa moja. Sasa, wakati mwingine unapomwamini Mungu, inakufanya utende kipumbavu sana kwa watu. Unaweza kuwazia, mzee sasa, huyu hapa Musa sasa mwenye umri wa miaka themanini, naye amejificha huko nyuma jangwani kutokana na kazi ambayo Mungu alikuwa amemtuma kufanya. Lakini, alipofika kwenye mchanga huo mtakatifu wakati mmoja, ambapo wanasayansi wasingeweza kulielezea vinginevyo kwake . . .

107 Hakuna mtu anayepaswa kuihubiri Injili mpaka kwanza awe amekutana na Mungu kwenye mchanga mtakatifu, ambapo hakuna mtu anayeweza kumpokonya; ibilisi hawezi kukanyaga ardhi hizo takatifu. Wewe ulikuwepo wakati lilipotukia, nawe unajua unachozungumzia, haijalishi ni *hii* ngapi ya kisayansi, na ni *ile* ngapi.

108 Vipi kama Musa angelisema, "Ninaamini nitakwenda na kuchuma baadhi ya majani kutoka kwenye ule mti, nishuke kwenda kwenye maabara, na kuyafanyia uchunguzi, nione ni kwa nini hayateketei"? Mungu asingezungumza naye kamwe, bali aliketi tu chini na kuzungumza Nayo.

109 Hiyo ndiyo njia ya kufanya, kuketi chini moja kwa moja na kuzungumza na Mungu, atakujibu. Loo, wakati mwingine unapofanya hivyo, inakufanya utende mambo kigeni kwa ulimwengu wote.

110 Kesho yake, huyu hapa mzee sasa, mwenye umri wa miaka themanini, masharubu yakining'inia chini namna *hii* na kichwa chake chenye upara kiking'aa, mkewe ameketi kwa kutagaa juu ya nyumbu na mtoto mchanga nyongani mwake, namna *hiyo*, na fimbo mkononi mwake. Huyu hapa anashuka, akipaza sauti, "Utukufu! Haleluya! Nashuka kwenda Misri kuiteka."

"Ati unaenda wapi, Musa?"

"Nashuka kwenda Misri kuiteka." Uvamizi wa mtu mmoja. Huo ni ujinga. Lakini, ilikuwa nini?

"Musa, aisee, Ndugu Musa, kwani unaenda wapi?"

111 "Nashuka kwenda Misri, nashuka kwenda kuiteka." Kama tu, uvamizi wa mtu mmoja akienda kuiteka Urusi. Mnaona? Ile kuu, ilikuwa imeishinda dunia nzima, lakini, "Ninashuka kwenda kuiteka," akiwa na fimbo mkononi mwake.

"Utaifanya na nini, Musa?"

112 "Mungu alisema, 'Shika fimbo hii uendelee mbele.' Kwa hiyo, mimi huyu hapa ninaenda." Uvamizi wa mtu mmoja, upuuzi kwa akili ya kimwili. Lakini, alifanya hivyo. Kwa nini? Mungu alisema hivyo. Amina. Hilo latosha.

113 Ninaweza kuona baadhi ya makuhani wakisimama na, Wamidiani, nao wakisema, "Sasa, ngoja kidogo, Ndugu Musa, umekuwa mchunga-kondoo mashuhuri uliyefanikiwa hapa, hupaswi kutenda kijinga namna hiyo."

114 "Lakini, unaona," akasema, "Nilikutana na Mungu, naye Mungu akaniambia niende kufanya hivyo," naye akalifanya. Ambapo utafiti wake wa kisayansi na kila kitu kilikuwa kimeshindwa, Neno la Mungu haliwezi kushindwa, kwa hiyo, Musa aling'ang'ania. Alimwua Mmisri mmoja, kisha akatoroka kwa sababu ya vitisho vya watu; naye akashuka kule, baada ya hayo, na kuliua taifa zima, akiwa na fimbo iliyopinda mkononi mwake.

115 Unaona, Mungu hufanya mambo ya kipumbavu sana kwa nia ya kimwili ambayo haijui lolote juu ya Mungu, bali wanafikiri wanamjua. Mnaona? Mbona, Mungu huucheka ujinga wao. Lakini Yeye huwachukua wanyenyekevu wa moyo ambao watasikiliza, na kuzingatia kile anachosema. Ilikuwa ni ujinga, lakini Mungu alifanya hivyo.

116 Musa aling'ang'ania. Ati umzuie? Aliitupa fimbo yake chini, kama tulivyosema jana usiku, ikageuka ikawa nyoka, halafu jamaa hawa wengine wakatupa fimbo zao chini nazo zikageuka kuwa nyoka. Aling'ang'ania, akasimama pale na kusema, "Mungu wangu alinituma, ana uwezo wa kulirekebisha jambo hilo." Nyoka wake akawameza hao wengine, akasema, "Haya basi." Amina. Naam, bwana.

117 Aling'ang'ania kwa sababu alikuwa amemsikia Mungu, alikuwa na imani katika yale ambayo Mungu alisema yalikuwa kweli, kwa maana yalikuwa ni Maandiko. Mungu alikuwa ameahidi jambo hilo kwa Maandiko.

118 Unapomwona Mungu akiahidi chochote, na kisha ageuke nyuma na kuthibitisha aliyoyaahidi, basi unaweza kung'ang'ania. Hmm, nini kingeweza kutokea? Kama watu wangeweza kamwe kushikilia, na kufungua hisia zao zilizokufa

ganzi mbali na Mungu, na kuja waingie katika Roho Mtakatifu, na kumshika, na waone hapo ya kwamba ni Mungu, Yeye aliahidi jambo hilo.

119 Baadhi yao hawana hata ufahamu wa kawaida. Hiyo ni kweli. Watu, wao, baadhi yao wataninii tu. . . hawaamini hivyo kamwe, hakuna njia kwenu ya kuwaambia, kwa sababu walichaguliwa hukumu hiyo tangu zamani. Biblia ilisema hivyo, katika Yuda, ilisema, "Watu wa zamani, walioandikiwa tangu zamani hukumu hii, wabadilio neema ya Mungu kuwa ufisadi." Kweli kabisa! Je, si lingekuwa ni jambo la kutisha kujua kwamba ulikuwa ukisoma na kusikia ukihubiriwa Biblia, na halafu hukuiamini? Ni jambo la kutisha jinsi gani . . . hilo ndilo—hilo ndilo jambo la kutisha sana nijualo, ni watu ambao hawataliamini Neno la Mungu.

120 Sasa, Daudi, Daudi alikuwa mvulana mdogo wa kombeo kule nyuma, alikuwa na kombeo mkononi mwake, naye alikuwa akiwachunga kondoo wa baba yake. Simba akaingia, na kumchukua mmoja, na kutoka mbio, naye akamtumaini Mungu na kumwua huyo simba kwa kombeo, dubu akaingia na kumchukua mmoja, akamwua huyo dubu.

121 Kisha siku moja, alikuwa kule karibu na jeshi la Bwana, akiwapelekea ndugu zake zabibu na—na kadhalika wapate kula, sambusa, labda, alizopika mama yake. Na wakati akiwa huko, upande wa pili kulikuwa na Wafilisti, na huko walikuwa na Go—Goliathi, jitu kubwa mno la mwanaume, vidole inchi kumi na nne, amesimama huko nje, kasema, "Nitawapa pendekezo," hivyo ndivyo ibilisi afanyavyo anapowazia anakuzidi kidogo. Akasema, "Nitawapa pendekezo ninyi watu. Tusiwe na umwagaji damu. Sasa, acheni mtu mmoja ajitokeze na kupigana nami, wakiniua, basi nchi yangu yote itawatumikia ninyi, halafu basi, nikiwaua, basi nchi yenu itatutumikia." Loo, hakika, Shetani alifurahi kufanya majadiliano kama hayo, kwa hiyo, alijua hakuna mtu angemshinda.

122 Na huko, Sauli, mtumia mkuki aliyefundishwa vyema, shujaa tangu ujana wake, akiwa amesimama pale tangu kichwa hata mabega yake kwenda juu alikuwa mrefu kuliko jeshi lake, huko nyuma kabisa aliogopa kukutana naye. Lakini siku moja, alifanya—alifanya hivyo wakati m—mtu afaaye alipokuwa amesimama karibu, mvulana mdogo mwenye mabega yaliyoinama, Biblia ilisema, mvulana mwekundu amesimama pale, Daudi.

123 Naye akawageukia, akasema, "Mnataka kuniambia kwamba ninyi, jeshi la Mungu aliye hai, mtasimama hapo na kumwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa ayatukane majeshi ya Mungu aliye hai?" Kasema, "Nitakwenda kupigana naye, ikiwa hamna ujasiri, nitaenda." Mungu sikuzote amekuwa na mtu mahali

fulani, mwenye ujasiri ambaye atasimama na kusema Kweli, na kulifuatilia.

Alisema, “Ni—nitakwenda kupigana naye.”

“Mbona,” wakasema, “wewe si chochote ila kijana, naye ni nanii . . . tazama, mbona, wewe angalau si mkubwa kama mkono wake.”

Akasema, “Hiyo haileti tofauti yoyote.”

124 Kwa hiyo, ikamfikia Sauli, ndipo Sauli akapanda kule, akasema, “Sasa, Daudi,” akasema, “Napenda ujasiri wako, mwanangu, lakini huna uzoefu wowote wa mapigano, kwa hivyo labda afadhali uvae jaketi langu,” akavaa silaha zake na kidogo zikamlemea maskini Daudi.

125 Inanikumbusha, alikuja kugundua kuwa jaketi lake la kikanisa halikumwenea mtu wa Mungu. Ndivyo ilivyo siku hizi, unajifunza Ph.D. yako, LL.D. yako, na jinsi ya kupambana na kanuni za imani, na kadhalika, asingalipigana naye kamwe.

“La,” akasema, “niondoleeni mbali kitu hiki,” kasema, “Sijapata kukithibitisha bado. Acheni niende na kile ninachojua Mungu amebariki.” Amina.

126 Mungu anawajibika kwa Neno Lake. Kweli. Acha niende na Neno la Mungu. Mungu aliahidi kubariki Neno Lake, wala halitamrudia bure. Haidhuru ni wangapi wanaojaribu kukufukuza, kaa papo hapo kwenye hilo Neno, Mungu aliahidi atashughulikia hali hiyo.

Daudi akasema, “Nitakwenda kupigana naye.” Loo, jamani! Aling’ang’ania.

Ndugu zake wakasema, “Najua wewe ni mtukutu. Rudi kwenye mbwa wako na kwa hao kondoo kule kilimani.”

Lakini, Daudi asingefanya hivyo, kwa maana Mungu alikuwa ametia nanga tayari. Akasema . . .

“Mbona,” akasema, “mtu huyo atakuchoma kwa mkuki wake,” na yote atakayofanya, na yote namna hii.

127 Akasema, “Lakini, nilikuwa nikichunga kondoo wa baba yangu, naye Mungu akanisaidia kutoa mwa—mwana-mbuzi kutoka katika kinywa cha simba, na dubu,” na kadhalika. Naye akasema, “Mungu ambaye angechukua . . . angeacha . . . angenipa ukombozi kutoka kwa makucha ya simba huyo na makucha ya dubu huyo, ni zaidi sana jinsi gani Yeye atanipa ushindi juu ya huyo Mfilisti asiyetahiriwa, anayetukana, akisema, ‘Siku za miujiza zimepita,’” hiyo kanuni kubwa ya imani ya kimadhehebu inayojaribu kuisukumia miujiza ya Mungu nyuma kabisa *hapa* ndani, na uponyaji wa Kiungu katika ule Utawala wa Miaka Elfu Moja, wakati mtakapokuwa wasiopatikana na mauti. Mungu ni yeye yule jana, leo na hata milele. Kama kuliwahi kuweko na Mungu, Yeye angali ni Mungu.

Hakika. Huyo hapo. Nanyi mnajua kilichotukia katika hiyo hadithi. Naam.

128 Yohana Mbatizaji, alipojitokeza. . .Sasa, hatuna kumbukumbu nyingi za Yohana. Alikuwa mwa—mwana wa kuhani, ila kamwe hakulifuata hilo dhehebu pamoja na baba yake, hakufanya hivyo, alikuwa na kazi muhimu, alikuwa ndiye yule atakayeitwa katika historia kumtangaza Masihi. Alikaa nyikani mpaka alipokuwa na uhakika, mpaka Mungu alipokutana naye. Hakushuka na kujipumbaza na kanuni zao za imani na kadhalika walizokuwa nazo, kusomea kuwa makuhani na kadhalika; alienda huko nyikani na kuishi kwa nzige na asali mwitu, wala hakuomba chochote kutoka kwa mtu yeyote, bali alikaa pale. Ndipo Mungu akasema naye siku moja na kusema, "Sasa, utamjua Masihi huyu. Sasa, ajapo, mtu yeyote utakayemwona Roho akimshukia na kukaa ndani, huyo Ndiye niliyemwita, Yeye Ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu na moto."

129 Sasa, kama Yohana angalishuka, na kupata ujuzi wake wa seminari na kila kitu, aingie ndani, D.D. kubwa, mwajua. Baadhi ya madaktari wa kiungu wangesema, "Yohana, tunaelewa, kulingana na kuzaliwa kwako huko nyuma, kwamba ulichukuliwa mimba katika mama yako wakati alipokuwa, mwanamke mkongwe na—na kadhalika. Na sasa, wewe, hapana shaka ila utakuwa ndiye yule atakayemtambulisha Masihi. Ulisema utakuwa ndiye 'sauti ya mtu aliaye nyikani.' Hivi hufikirii kwamba Dk. Jones hapa ndiye huyo jamaa? Loo, mwangalie, jinsi anavyoweza kuninii tu. . . " Loo, unaona? Mbona, huenda angalishawishiwa, lakini Yohana alijiepusha na upuuzi huo wote. Akakaa nyikani mpaka aliposikia kutoka kwa Mungu.

130 Loo, laiti watu wangaliondokea upuuzi huu wote, "Siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu," na wawe peke yao mahali fulani, na kukaa pamoja na Mungu mpaka uisikie hiyo Sauti ikisema, "Mimi ndimi Bwana Mungu wako, niponyaye magonjwa yako yote; yeye yule jana, leo, na hata milele." Hapo ndipo unapompata Mungu.

131 Sasa, yeye alikuwa na hakika sana, aling'ang'ania sana, hata akasema jambo hili, alijua ya kwamba Masihi angetokea katika kizazi chake, akasema, "Kuna Mtu aliyesimama kati yenu sasa hivi ambaye hamumjui." Alijua alikuwa duniani papo hapo, kwa maana yeye angemtambulisha. Loo, aling'ang'ania, bila shaka.

132 Maskini Samsoni aling'ang'ania alipotoka kule, na hapo. . . Mtu amemfanya Samsoni. . .Niliona picha wakati mmoja ya Samsoni kwenye jumba la makumbusho la Kiyunani, na ule uumbaji. Ilikuwa ni ujinga, kuonyesha kile ambacho nia ya kimwili inaweza kuwazia wakati haijaongoka kwa Kristo. Hawa akiwa amesimama pale, mnyama mwenye sura mbaya sana

niliyepata kumwona. Loo, unafikiri ya kwamba Mungu, aliumba kitu kama hicho? La, bwana. Naye Adamu, alionekana kama jitu fulani cha zamani za kale, sijapata kuona kitu kama hicho. Mnajua, Mungu alimfanya mkamilifu. Mungu alim-. . . Hawa alikuwa ndiye mwanamke mrembo zaidi aliyepata kuishi, alikuwa ni mfano wa Mungu wa mwanzoni wa akina mama, bila shaka ndivyo ilivyokuwa.

133 Na hapo walikuwa na Samsoni mwenye mabega ukubwa wa—wa milango ya ghala. Sasa, haingekuwa ni jambo la ajabu kwangu kumwona mtu mwenye mabega kama hayo, mikono mikubwa namna *hiyo*, akinyosha mkono na kumshika simba, amrarue vipande-vipande, la hasha. Kumwona akiyanyanyua malango ya mji na kuondoka nayo; mbona, yeye ni mkubwa mara tatu kuliko hayo malango, anapaswa kuwa na uwezo wa kuondoka nayo, hakika, kulingana na hilo. Lakini Samsoni, ukitaka kujua, alikuwa ni maskini mduvi mdogo tu, maskini mvulana wa mama mwenye vishungi saba vya nywele vilivyoning'inia mgongoni mwake. Lakini, alikuwa Mnadhiri kwa Bwana. Amina.

134 Sasa, wakati simba alipokuja mbio na kumngurumia Samsoni, alikuwa hajiwezi, lakini, Roho wa Bwana akamshukia, njia ambayo Mungu angeweza kuitumia, yeye hakuwa jitu la kiakili, alitoka akaenda tu pale chini ya nguvu za Mungu na kumrarua vipande-vipande. Sasa, hiyo ni siri jinsi angeweza kufanya hivyo, jamaa mdogo kama huyo.

135 Basi siku moja alikuwa nje kondeni, ndipo Wafilisti elfu moja wakamzunguka. Sasa, helmeti hizo ni kama shaba yenye unene wa inchi moja na nusu, ambayo inaning'inia juu ya vichwa vyao. Hayo makoti makubwa ya kile wanachokiita daraya, yalipandana na chuma, wakati mwingine unene wa nusu inchi au zaidi, yalipandana mpaka chini, hivyo ndivyo walivyokuwa wamevalia, ngao kubwa sana hapa mbele ya miguu, na kadhalika. Kubwa. . .Loo, ingehitaji mtu-jitu kuzibeba, na kulikuwako na elfu yao wamesimama pale, nao wakamzingira Samsoni.

136 Jambo pekee alilopaswa kufanya ni kuangalia nyuma na kuhisi agano hilo pamoja na Mungu. Amina. Ndivyo hivyo. Basi akatafuta kitu fulani, na palikuwa na taya ya nyumbu imewe-. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . . Mfilisti. Alikuwa aking'ang'ania. Kwa nini? Alijua ya kwamba Mungu alikuwa amembariki; alijua Roho wa Mungu alikuwa juu yake, kile alichokuwa nacho mkononi mwake, alikitumia.

137 Loo, kama Uzao wa Ibrahimu siku hizi, wana wa Mungu, wangeweza kuchukua imani ndogo uliyo nayo, na kuwa mvumilivu nayo, Mungu ataitumia. Naam. Loo, ni. . .Ni—nikianza kuongea, naondoka kwenye somo langu.

138 Mwanamke huyu wa Kiyunani, alisikia. “Imani chanzo chake ni nini? Kusikia, kusikia Neno la Mungu.” Sasa, yeye alikuwa Myunani, kumbukeni, lakini mwajua, imani hupata chanzo ambacho hakuna kitu kingine kinachoona. Imani hupata chanzo chake ambacho jicho la mwanadamu halikioni, lakini hukipata hata hivyo. Neno Lake ni Upanga mkali wenye makali kuwili, Waebrania 4:12, na imani ambayo inaushika huo Upanga.

139 Sasa angalieni, kuna kila kitu hapa nje kukuweka mbali na kila baraka za Mungu. Sasa, mtu fulani angeweza kuinua imani kwa ninii mdogo, ama, Upanga kwa mkono mdogo, dhaifu na kukata kitu kingine kidogo kufanya ungamo.

140 Siku hizi, tunasikia mengi sana kuhusu maamuzi, “Tulifanya maamuzi *kadhaa*.” Maamuzi ni mawe, kama vile Petro, maamuzi. Lakini, kuna faida gani lundo la mawe kulundikwa pamoja, kama huna mwashi wa mawe hapo mwenye upanga mkali wenye makali kuwili kuyakata yawe wana na binti za Mungu?

141 Ndiyo sababu Billy Graham alisema huko Louisville, alienda huko na kuwafokea wahubiri hao, nilipokuwa nimeketi moja kwa moja pale katika kifungua kinywa chake, akasema, “Enyi wahubiri wavivu, ninaingia mjini,” tena kasema, “Ni—ninafanya uamsho na kupata waongofu elfu thelathini, ninarudi baada ya miezi sita, siwezi kupata thelathini.” Kasema, “Kwani kuna nini?” Kasema, “Paulo aliingia katika mji fulani, naye akampata mwongofu mmoja kisha akarudi miezi sita baadaye, naye alikuwa na hamsini juu ya huyo mmoja.” Kasema, “Alikuwa na wajukuu wa vitukuu wa vitukuu, tuseme, nyuma.” Akasema, “Ni ninyi wahubiri wavivu.”

Loo, nilitaka kusema jambo fulani kwa huyo mwinjilisti mkuu, bali nilikuwa mjinga tu, kwa hiyo niliketi tu kimya.

142 Basi, nataka kuuliza kitu: Ni mhubiri gani mvivu alishindwa kumchukua mwongofu wa Paulo? ikiwa ni wahubiri wavivu walioweka miguu yao juu ya dawati, na hawaendi kuwatembelea watu ambao walifanya kadi zao za uamuzi. Ni kwa sababu Paulo alichukua uamuzi huo na kukaa huko nao, mpaka alipoukata katika umbo la Yesu Kristo kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, nao ukawaka moto sana ukajifanya wenyewe, basi, kuwa mwingine, sio maamuzi, kwenda tu kusema, “Ninafanya uamuzi,” kaendelea moja kwa moja na ulimwengu wote.

143 Sasa, Billy alisema ya kwamba kati ya elfu thelathini, asingeweza kupata thelathini wakati mwingine. Ni kwa sababu kwamba, jambo pekee unalofanya ni kuyafingirisha hayo mawe. Afadhali hata uyaache tu shambani kama hutayakata, uyatengeneze yawe katika jengo la Mungu, kufanya wana na binti kutoka kwao katika. . .Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, nalo linakata. Basi *tohara* inamaanisha

nini? “Kata nyama ya ziada,” ulimwengu. Neno huitahiri, huikata.

144 Imani inashikilia Upanga huo, wengine wanaweza kukata vya kutosha kujiunga na kanisa, wengine wanaweza kuendelea na kuingia katika mambo ya kilindi, na wengine wanaweza kukata hata kufikia uponyaji wa Kiungu, inategemea huo mkono wenye nguvu wa imani unaotumia huo Upanga. Hiyo ni kweli. Inategemea . . .

145 Alikuwa na vizuizi vingi, mwanamke huyu alikuwa navyo. Loo jamani, ningeweza kutaja zaidi ya dazani moja, ama mbili, nilivyoandika hapa ambavyo vingemzuia. Lakini, imani yake haikuwa na kizuizi chochote.

146 Unaweza kuwa na kizuizi. Mchungaji wako anaweza kusema, “Ukihudhuria mkutano kama huo, nitakufukuza kanisani.” Vema. Hicho hapo kizuizi chako. Mume wako anaweza kusema, “Nitakuacha.” Mke wako anaweza kusema, “Sitaninii . . . Kamwe sitaninii . . . Ni—ni—nita—nitakutaliki.” Unaweza kuwa na vizuizi vingi, lakini, ikiwa una imani, haina kizuizi chochote, haijui chochote ila Neno la Mungu, na hukaa Nalo, hiyo ni kweli, Neno la Mungu.

147 Huenda walimwambia, “Wewe ni Myunani. Huyo—mtu huyo si wa dhehebu lako, wewe ni Myunani. Vema, kundi le—letu haliwafadhili,” chochote kile.

148 Kundi lingine huenda lilikutana naye, na kusema, “Mbona, siku za miujiza zimepita, hakuna kitu kama hicho. Kundi hilo la watakatifu wanaojibingirisha kule chini hawajui wanalozungumzia, hao Wayahudi. Sisi ni Wayunani, tuna akili, tumeelimika, tunajua mambo, lakini, sisi ni watu wenye akili, lakini hebu liangalie kundi lile la—la watu huko chini, yote wanayozungumzia ni Mungu fulani wa kimbinguni akifanya jambo fulani hivi, wakipitia Bahari ya Shamu, ama kitu kama hicho.” Mnaona? “Lakini, wewe ni Myunani, wewe ni mwerevu kuliko hivyo.” Lakini, imani ilishikilia, naye akang’ang’ania, akalipita hilo moja kwa moja, aliliamini.

149 Kisha akakutana na kundi la wanawake labda, nao wakasema, “Unajua nini, mpenzi, Martha Luella,” natumai hakuna mtu hapa kwa jina hilo, nilitaja jina la kigeni, “unajua, Martha Luella, kitakachotukia? Mume wako atakuacha kwa sababu yeye ni mfanyabiashara wa mjini, ukihudhuria huko chini huo uliko.” Hiyo inaleta tofauti gani? Mume au bila mume, alishikilia, aling’ang’ania, alijua alikuwa na haja ya Kristo, naye alikuwa anaenda kumwona, kwa sababu alikuwa amesikia ya kwamba Yeye ni Mponyaji, alikuwa anaenda kuona hilo. Hakika.

150 Huenda mwingine, anayefuata huenda alisema, “Sawa. Ukienda huko chini, utachekwa, mji mzima utakuita jina fulani baya, watakuita mtakatifu anayejibingirisha, ama Mpentekoste, ama chochote kile. Ukienda huko chini kati yao, hakika

utabandikwa jina." Aling'ang'ania, akaendelea mbele moja kwa moja, ndugu. Hakuna kitu kitakachomzuia mwanamke huyo. Naam, bwana.

151 Kisha huyo mwingine. Huyu hapa kuhani anakuja, alikuwa ndiye wa mwisho, kasema, "Ukienda, tutakutoa kanisani na kukutenga." Hilo halikumzuia hata kidogo. Imani chanzo chake ni kusikia. Alikuwa na haja, alishuka moja kwa moja kule chini, aling'ang'ania, alikuwa anaenda kumwona Yesu.

152 Na sasa, watu wengi wanafikiri punde tu wanapomwona Yesu, yote yamekwisha, "Utukufu kwa Mungu, nina ubatizo wa Roho Mtakatifu, sasa, nitalala tu na kustarehe." Mbona, wewe—wewe si mtawaliwa wa Roho Mtakatifu bado. Sikiliza, ulipompokea Roho Mtakatifu, papo hapo ndipo unapopata shida yako, hapo ndipo shida inapoanzia. Kweli kabisa. Hapo basi ndipo huna budi kupiga vita, hiyo ndiyo sababu ya Yeye kutolewa kwako, Yeye ni Upanga. Hiyo ni kweli. Hapo ndipo vita vyako vinapoanza.

153 Sasa, alikuja mpaka hatimaye akafika mahali Yesu alipokuwa. Sasa, alikuwa amepiga vita kupitia kila mojawapo ya vizuizi hivi, anayeng'ang'ania. Jamani, huyu hapa anakuja, akipenya kupitia, "Siku za miujiza zilipita, kukucheka, mumeo kukuacha, kutengwa na kanisa," *mengine mengi*, "kuitwa mtakatifu anayejibingirisha," au *mengine mengi*. Yeye, aling'ang'ania tu, anakuja, sasa anakutana na Yesu, kasema, "Sasa nimeipata, sasa niko Mbele Zake."

154 Basi angalia, mara tu Yeye . . . alipokutana Naye alikabiliana na sikitiko lingine. Naam. Alisema, "Sijatumwa kwa jamii yako." Loo, Mungu yeye yule aliyekuwa akimheshimu! Na yale aliyoyasalimisha? Kanisa lake na kila kitu alichokuwa nacho.

155 Alikuwa na binti, alikuwa mahututi sana, alikuwa na kifafa, naye alikuwa akijaribu kumfikia Yesu, maana alijua alikuwa amewaponya wengine. Kwa hivyo, kwa nini asiweze, kumponya binti yake? Kwa hiyo, yeye . . . Baada ya kuacha, kila kitu alichokuwa nacho na kumwendea Yeye, halafu hilo sikitiko, kuaibishwa tena. "Sijatumwa kwa jamii yako, nimetumwa kwa wana wa Israeli pekee."

156 Lakini, mwajua nini? Hilo haliizuii imani yake. La, bwana. Alitia bidii moja kwa moja tena. Akamtaja kama "Mwana wa Daudi." Hakuwa "Mwana wa Daudi" kwake. Lakini, aliposema, "Bwana," hiyo ilikuwa tofauti, alikuja kwa njia ifaayo basi. "Bwana, unirehemu!"

157 Akasema . . . Jambo lingine, akasema, "Nyinyi si kitu ila kundi la mbwa. Sijatumwa kwenu." Angalia yale maskini mwanamke huyo mdogo alikuwa amefanya, mambo aliyokuwa amepitia, kila kitu kilichomlazimu kusukuma apate kumfikia Yeye, na halafu, alipofika Kwake, Yeye alisema, "Sijatumwa kwa

jamii yenu, nanyi si kitu ila kundi la mbwa." Hmm! Jamani, jamani!

Bado aling'ang'ania. Hakika. Kwa nini? Alikuwa na imani. Loo, baada ya Yeye . . .

158 Hilo halingefanya kazi kwa kundi la Wakanada, sivyo? au kundi la Wamarekani. Ukiwaita mbwa, au kitu kingine, "Mbona, ninyi ni—ninyi ni *ninii,* nyinyi ni kundi la Waanglikana, ninyi ni bure," kitu kama hicho. Loo! Masalaale. Wewe, ulilipuka kama chura aliyepigwa risasi. Na kisha, usingekuwa . . . Kwa nini, jamani! Usingefanya hivyo, kuninii . . . Kunradhi kwa tam- . . . , au, tamshi. Sikupaswa kusema hivyo. Samahani. Lakini ungekuwa—ungewazia vibaya sana kuhusu hilo.

159 Kama Yesu angalisema, "Sijatumwa kwenu Waanglikana. Sijatumwa kwenu Wapentekoste. Ninyi ni kundi, ninyi ni Assembly of God, ninyi Church of God, ninyi, chochote kile mlicho, sikutumwa kwenu, ninyi si kitu ila kundi la mbwa." Loo, jamani!

160 Nilikuwa nimeona sura hiyo ya masikitiko, na kusema, "Vema, sitakuwa na uhusiano wowote Naye hata kidogo, kwanza kabisa hakuwa sahihi. Nitarudi tu kwenye kanisa langu mwenyewe."

161 Lakini si yeye, alikuwa na imani. Yeye hakuwa mmea wa tuta, chotara, kama baadhi yao siku hizi wanaojiita waaminio, hawawezi kutulia hata dakika moja kwa Injili. Hao ndio tulio nao siku hizi, lundo la mimea ya tuta, huna budi kuwabembeleza kila wakati, kuwanyunyizia sikuzote, kuwaondolea wadudu. Kweli. Kuwabembeleza kama mtoto wa paka, ukiyapapasa manyoya yake kwa njia moja, atakoroma, lakini hebu yapapase kinyumenyume mara moja, ndipo ataonyesha kilicho ndani yake. Hiyo ni kweli. Bila shaka ni kweli.

Yeye hakuwa tu- . . . chotara. Chochote ambacho ni chotara ni aibu. Chotara hana . . .

162 Mbona, wao . . . Niliona . . . Nilisoma makala kwenye *Reader's Digest* hivi majuzi, ambapo wananinii, kama wakiendelea kuotesha mahindi chotara na mambo kama hayo, wanawake hata hawataweza kupata watoto miaka ishirini kuanzia leo. Yanairarua tu jamii ya wanadamu vipande-vipande na kusababisha kansa, na chochote kile. Ni chotara, hayafai. Wanasema, "Loo, chukua ya Funk," au chochote kile, mahindi chotara, "ni bora zaidi." Ni kitu cha kupendeza, nafaka kubwa mno, nzuri sana, lakini haina chochote, hebu ipande tena, wala hata haitafanya chochote, haiwezi kujizaa yenyewe. Hakuna kitu chotara . . .

163 Hebu mchukue nyu—nyu—nyumbu; nyumbu ni chotara. Yeye ni nini? Baba yake alikuwa farasi dume, mama yake alikuwa pu—punda jike. Na huyo . . . Yeye ndiye mjinga zaidi aliyepo, atasubiri maisha yake yote apate kukupiga teke kabla hajafa.

Huwezi kumwambia chochote, huwezi kumfundisha chochote, anaketi tu na hayo masikio makubwa, marefu, "Hoo, hoo," anaenda, anazungumza juu ya "siku za miujiza zimepita. Hoo, hoo, hoo, hamna kitu, zimepita." Mnaona?

164 Lakini, loo, farasi mzuri ukoo safi! Naam, bwana. Kuna dini nyingi sana za nyumbu siku hizi, kundi ambalo hata halijui wanakoelekea. "Je, wewe ni nani, Mkristo?"

165 "Mimi ni Mmethodisti; mimi ni Mpresbiteri; mimi ni Mpentekoste; mimi ni *hili*, *lile*, au *linginelo*," chotara. Haliwezi kujizaa lenyewe. Dhehebu lolote ni chotara, haliwezi kujizaa tena, limekufa linapofanya hivyo.

166 Lakini farasi mzuri, asili bora, ukoo safi, anaweza kukwambia baba yake alikuwa nani, mama yake alikuwa nani, babu yake, bibi yake, huko nyuma kabisa. Na Mkristo halisi, mzuri, ukoo safi, aliyezaliwa mara ya pili, kwa Roho Mtakatifu, anaweza kurudi moja kwa moja kwenye Siku ya Pentekoste. Haleluya! Unaweza—unaweza kusema, "Yesu Kristo, ni yeye yule jana, leo, hata milele," huyo jamaa ukoo safi atapaza sauti, "Amina! Haleluya!"

167 Chotara, dini chotara, loo, inaonekana kuwa nzuri zaidi, hakika. Makanisa makubwa mno, mazuri na mamilioni ya dola ndani yake, na kadhalika namna hiyo. Naye mhubiri anaweza kusimama na—na kunena hivyo, takriban dakika kumi na tano tu juu ya jambo lile lile unalotaka azungumzie, maua, ama kitu kingine, ama siasa fulani, kisha arudi. Nawe unaweza kuwa mfuasi wa kanisa na kucheza karata, kuvaa kaptura, kufanya chochote unachotaka, uishi kama ulimwengu, unafikiri hiyo ni sawa, huo ni uchotara wako, lakini inapofikia Uzima, haupo.

168 Kwa Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, mtu aliyezaliwa mara ya pili hatakwepa Neno moja la Mungu, Mkristo aliyezaliwa mara ya pili ataambatana na yale Neno lisemayo.

169 Hakuwa chotara, hakuwa mmea wa tuta, imlazimu kubembelezwa. Na, kama mhubiri akihubiri zaidi ya dakika kumi. . .Baadhi yao wataenda kanisani, na kuketi mkutanoni, ukisema jambo moja wasiloamini nao, "Hmm, nitatoka hapa sasa hivi." Hiyo hata si adabu ya kawaida. Hiyo ni kweli. Hiyo inaonyesha ulichoumbiwa, hiyo inaonyesha ukoo wa watu.

170 Kama nilienda katika kanisa la Katoliki ya Kirumi, ama kwenye—kwenye, popote nilipoenda, ningekuwa na adabu ya kukaa na kusikiliza hadi jambo hilo litakapokwisha. Hiyo ni kweli. Lakini machotara siku hizi, mnaona, wa—wanakiri kumjua Mungu. Yesu alisema, "Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake: hao nao ujiepushe nao. Kwa maana hao ndio waendao nyumba kwa nyumba, na kuwaongoza wanawake wajinga, waliochukuliwa na tamaa za aina nyingi," wanawake wa kila namna.

171 Mwanamke mmoja aliniambia huko chini Marekani, hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikilikemea kanisa kwa vile walivyokuwa wakifanya, alikuwa, maskini nguo ndogo, akionekana mtovu sana wa uadilifu namna hiyo, naye akasema, “Vema, sasa, sikiliza hapa, Bw. Branham,” akasema, “Mimi ni Mmarekani, na hayo ni majaliwa yangu niliyopewa na Mungu.”

Nikasema, “Huenda ikawa ni majaliwa yako uliyopewa na Marekani, bali si majaliwa yako uliyopewa na Mungu.”

Akasema, “Vema, huwezi kununua nguo zingine isipokuwa hizo.”

Nikasema, “Ngoja nikwambie kitu, dada, wangali wanauza cherehani na vitambaa, kwa hivyo usiwahi kutoka nje ya hilo.” Mnaona?

172 Ni kwa sababu tu tamaa mbaya iko ndani ya mioyo ya watu. Ikiwa wamezaliwa mara ya pili, hawatataka kufanya jambo hilo. Laiti tungalikuwa na wahubiri mimbarani, ambao wangevua glavu hizo za kikanisa, na kulitapanya Neno hilo huko nje, na kuwaambia ukweli, na kukata vibanzi, na kuviacha vianguke vitakako, lakini jambo ni kwamba, sisi . . . Hiyo ni kweli.

173 Hiyo ndiyo sababu hatuoni ishara na maajabu, na yanapotokea, yanayashangaza makanisa, hawajui la kufanya, na kurudi nyuma kama walivyofanya siku zile, kasema, “Ni Beelzebuli, ibilisi.” Mnaona? Hawajui kabisa.

174 Afadhali nisimame na kuendelea hapa. Vema, hata hivyo, sitaki kuwadhuru, lakini nataka kunyoa kidogo tu, ili mjue mnaposimama. Mtakapokutana nami kwenye Kizimba cha Hukumu, mtaliwajibikia. Kumbukeni tu, mtawajibika, kwa sababu ninawaambia Ne—Neno, Neno la Mungu hasa.

175 Sasa, alikiri ya kwamba Yeye hakutumwa kwa jamii yake; alikiri kwamba hakuwa kitu ila mbwa. Loo, tungefanya hivyo? Loo, la, la hasha. Unasema, “Mimi hufanya nipendavyo.” Endelea, nenda tu moja kwa moja kanisani, ukitaka, hiyo ni sawa, lakini kumbuka, utakabiliana nalo tena siku moja. Ulimwengu umechafuliwa na upotovu, kitu chote, Biblia ilisema hivyo, elimu, ustaarabu uliingia.

176 Wakati ninyi Wahindi mlipoimiliki nchi hii wenyewe, hapakuwa na shida kati yenu. La. Mliishi maisha mazuri, marefu, na kila kitu kiliendelea vizuri. Ugomvi mdogo-mdogo wa kikabila mlisuluhisha kwa kutoka huko nje na kupigana kati yenu, lakini wakati mzungu alipoingia, alileta wanawake, wiski, unywaji pombe, dhambi, nao ustaarabu uliopotoka daima husababisha hilo. Mna nini? Upotovu, mauaji, wizi, unyang’anyi, ushoga, mambo ya kila namna siku hizi za mwisho, yale hasa Biblia ilisema yangetukia, lakini hapa tunayo. Mnaona? Si ajabu mtu hawezi kung’ang’ania, hawajui wanakosimama. Chotara anawezaje kung’ang’ania wakati hata hajui baba na mama yake ni nani. Mnaona? Usingeweza kufanya hivyo.

177 Sasa hebu nikwambie jambo fulani, mama, sikiliza tu hili, dada, humu ndani: Wewe endelea na kufanya utakavyo. Lakini, unavaa hizo nguo za kizinifu, na kutoka hapa mtaani, unawaweka binti zako huko nje namna hiyo, na mwanamume fulani anamtazama kwa njia isiyofaa, unaweza kuwa safi kama yungiyungi, unaweza kuwa na heshima kwa mumeo uwezavyo kuwa, au kwa rafiki yako mvulana, lakini kwenye siku ya hukumu utawajibika kwa kufanya uzinzi, maana Yesu alisema, "Kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake." Mwenye hatia ni nani? Wewe ulijianika mwenyewe, una hatia.

178 Na halafu mhubiri huyo chotara anasimama mimbarani, na anaona haya kuwaambia watu. Ni njia ya kujipatia riziki, hawana budi kufanya hivyo wapate kushikilia haki zao za kimadhehebu, na makanisa yao makubwa, na kadhalika.

179 Tunachohitaji leo hii ni watu halisi wa Mungu, wanaosimama juu ya Neno hilo na kusema ukweli juu Yake. Hiyo ni kweli. Kumbukeni, kutakuwa na wachache tu watakaookolewa kwa vyovyote vile, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ambapo watu wanane waliokolewa, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

180 Sasa tazama, alikiri, i—i—imani halisi ya kweli sikuzote hukubali kwamba Neno ni la kweli, sasa angalieni, sikuzote akikubali Neno ni la kweli: "Kweli, Bwana, mimi si kitu ila mbwa. Kweli, Bwana, kamwe hukutumwa. . .Hukutumwa kwa jamii yangu. Hiyo ni kweli." Hakutaka kuona *hili* lilikuwa ni nini, ama *lile* lilikuwa nini, alikiri tu kwamba Neno lilikuwa kweli. Naye Roho wa imani daima hukiri kwamba Neno ni sahihi. Angalieni, "Kweli, Bwana. Sitafuti mkate wa watoto, lakini hebu niokote tu makombo yanayoanguka kutoka kwenye meza ya Bwana, makombo tu."

181 Hilo likampata, jambo ndilo hilo. Akasema, "Kwa msemo huu wako. . .nenda zako, binti yako amepona." Imani hukubali ukweli. Vile vile sasa, imani daima huendana na Neno. Aling'ang'ania, naye akapata alichoomba bila kujali hali ya mambo.

182 Martha, akiwa Mbele za Yesu, aling'ang'ania, alisimama pale, naye akaamini. Na haidhuru, ingawa kaka yake alikuwa amekufa siku nne na sasa ananuka, alisema, "Bwana, amekufa, ananuka, lakini hata sasa, lolote utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa." Aling'ang'ania.

Hapo ndipo hatupati chochote, hatung'ang'anii. Sisi, hatuna imani, hatushikilii.

183 Yule mwanamke Mshunami alikuwa aking'ang'ania mbele ya Eliya. Akasema, "Kweli, hiyo ni kweli." Kasema, "Ulinibariki na mtoto akaja. Huyo mtoto amekufa." Lakini kasema, "Sasa,

sitakuacha, hakika kama vile nafsi yako haifi kamwe, na Bwana Mungu wako yu hai, sitakuacha,” mpaka akapata jibu kwa ajili ya mtoto wake. Aling’ang’ania. Imani hulishikilia Neno.

184 Mikaya, akisimama pale mbele ya manabii mia nne, wote wamelishwa na kunadhifishwa na kuvaa sare zao, na wamevalishwa. Naye Mikaya . . .

185 Akaja Yehoshafati, yeye alikuwa mwaminio, ama, mtu wa Mungu, akaja pamoja na Ahabu, alipaswa kujua kufanya vizuri kuliko hivyo, lakini alipofanya hivyo, alisema, “Hivi Ramoth-gileadi si mali yetu?” Sasa, angalieni hizo sababu, Ramoth-gileadi, Yoshua, katika kuigawanya hiyo nchi, aliwapa hiyo Israeli, Wafilisti wakaja na kuwanyang’anya.

186 Na sasa, Ahabu akasema, “Hivi Ramoth-gileadi si ni mali yangu?” Mwaminio huyo vuguvugu, mkwamia mpakani akasema, “Je, si mali yetu hiyo?” Kisha akasema, “Hiyo ni yetu.”

187 Naye Yehoshafati, akiwa katika kundi baya, akiketi katika umati mbaya ambamo hamkuwamo na imani, hawaliamini Neno la Mungu, akasema, “Mbona, inaonekana hivyo,” kasema, “lakini hivi hatupaswi kumwuliza Bwana?”

188 “Loo,” Ahabu akasema, “hakika, nina manabii mia nne hapa chini.” Akawaleta huko kila mmoja, manabii wazuri, waliovalia vizuri, manabii wa Kiebrania, simaanishi manabii fulani wa sanamu, walidai kuwa wanadini halisi wa Mungu wanayemtumikia, manabii.

189 Angalieni tu hapa, ni—nitachukua muda wangu papa hapa kwa dakika moja, manabii halisi, manabii wa Kiebrania, walikuja kule, na wote wakatabiri, nao wakasema, “Kwea, kwa kuwa Bwana atakwenda pamoja nawe. Nchi hiyo ni yetu kabisa, na mahindi hayo yanayokuzwa huko yanapaswa kuwa ya kuwalisha watoto wetu, badala yake, yanamlisha adui yetu; kwea ukawasukume kutoka humo nchini.” Sasa, hilo si linasikika la busara? Mungu aliahidi hiyo ilikuwa ni nchi yao. Na kwa hiyo, lakini basi, Mikaya akasema . . .

Vema, walisema . . . Kwanza, hii . . . Kasema, “Unaweza . . . Je, hakuna mtu mwingine tunayeweza kumwuliza? Je, hakuna nabii mmoja tu zaidi?”

190 Akasema, “Kuna mmoja, Mikaya, mwana wa Imla, lakini namchukia.” Hakika. Mtu yeyote ambaye angemwambia ukweli na kumfokea atoke dhambini mwake, alimchukia. Kasema, “Namchukia.”

Akasema, “Mfalme asininii, hivyo . . . asiseme hivyo.”

191 Ndipo shirika la wahudumu likaenda kule likakutana naye, naye kasema, “Mikaya, wahudumu hao wote, umefukuzwa kwenye hilo dhehebu sasa, wahudumu hao wote watakurudisha moja kwa moja ndani tena, kama utasema jambo lile lile yeye . . . wanalosema.”

192 Akasema, “Kama Bwana Mungu aishivyo, nitasema tu yale ambayo Mungu ataweka kinywani mwangu.” Haya basi. Huyo hapo mtu wa Mungu. Alikuja pale, akasema, “Nipeni usiku wa leo.” Akazungumza na Bwana, Bwana akamwambia, kisha akalinganisha ono lake na Neno.

193 Sikuzote linganisha mawazo yako na maono yako na Neno. Kama yanaambatana na Neno, Mungu aliyasema. Yasipoambatana na Neno, afadhali uwe mwangalifu.

194 Kwa hiyo, akalilinganisha na Neno. Mungu aliambia. . . Alisema aliona ono. Aliona jeshi la Mbinguni limeketi pamoja, na wote walikuwa wakisema, “Tungewezaje kumpeleka Ahabu kule tukamwue ili kutimiza Neno la Mungu?” Kwa maana nabii, Eliya, alikuwa amesema mbwa wangeilamba damu yake na kumla Yezebeli, naye, atatapanywa kondeni. Na mbona, hakika. Wakasema, “Tunawezaje kufanya hivyo?”

195 Ndipo pepo wa uongo akapanda kutoka chini na kusema, “Nitashuka na kuwaingia manabii hao, maana hawajui Neno kwa vyovyote vile. Kwa hiyo, nitashuka niende kule, na kuingia ndani ya hao manabii, na kuwafanya watoe unabii wa uongo, na kumpeleka kule.”

196 Kisha Mikaya akageuka. . .akaona hilo lilikuwa sawa kabisa na Neno la Mungu. Basi akaenda, akasimama mbele yake, naye akamwambia hayo. Na kwa hiyo, mnajua, Mikaya. . . Yule askofu mkuu akajitokeza, na kumpiga kofi usoni, kasema, “Neno la Mungu lilipitia njia gani, Roho wa Mungu, alienda wapi alipotoka kwangu?”

Akasema, “Utaona wakati umejificha nyuma ya kuta huko nyuma.”

Kwa hiyo akasema, “Mchukueni, mkamtie gerezani,” akasema Ahabu. Kisha kasema, “Nitakaporudi, nitamshughulikia jamaa huyu.”

Kasema, “Ukirudi kamwe, Mungu hajasema nami.”

197 Kwa nini? Akiwa amesimama pale alipoweza, kupigwa akafa. Lakini aling’ang’ania, alikuwa na Neno la Mungu. Alijua maana yake. Naam, bwana, alijua maana yake.

198 Filipo aling’ang’ania alipomsikia Yesu akimwambia mahali alipokuwa kabla hajamwita. Petro aling’ang’ania alipomwambia jina lake ni nani. Loo, jamani! Yule mwanamke kisimani aling’ang’ania.

199 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa huko chini Meksiko, nikifanya mkutano, na kulikuwako na ma—maskini mwanamke wa Kimeksiko, kulikuwako, nakisia mambo elfu nne ama tano ya ajabu yalikuwa yamefanywa. Usiku uliotangulia, maskini mzee kipofu, Mmeksiko, alikuja jukwaani. Nilikuwa kule tu, sawa tu na mkutano huu hapa, siku tatu usiku, nasi tulikuwa tumeuchukua uwanja huo mkubwa wa michezo ya ng’ombe, na

kulikuwa na maelfu mara maelfu waliofurika kule. Baadhi yenu Assembly of God, nitawaambia ni nani aliyekuwa akinifasiria, mmoja wa watu wenu, Ndugu Espinoza, kule California, mkalimani wa Kimeksiko. Nasi tulikuwa tumesimama pale.

200 Ilibidi wakaribie. . .Kulikuwa na wengi sana mle ndani, wakanifunga kamba mikononi mwangu wapate kunishusha upande wa nyuma wa—wa—uwanja huo mkubwa. Basi wakati. . .Tulikuwa tumesimama pale jukwaani. Mvua ikinyesha, imenyesha siku nzima, maskini hao Wameksi-. . . hamna mahali pa kuketi, waliegemeana tu. Nasi hatuwezi kuketi dakika tano, tumehukumiwa, hivyo tu. Hakika. Hawangeweza. . .Wa—walikuwa wamekaa huko siku nzima, wameegemeana.

201 Usiku huo, wakati mstari wa maombi ulipoanza, nami nikaanza kuomba, kulikuwa na maskini mzee wa Kimeksiko aliyekuja, alikuwa amevaa matambara, alikuwa kipofu, nami nikamwangalia, na viatu vyangu, ningalimpa hivyo ila havingemwenea. Na maskini jamaa huyo mzee, pengine hajawahi kula mlo mzuri maishani mwake. Nikamkumbatia kwa mkono wangu, nikamwombea, maana inakubidi kuwahurumia watu, usipofanya hivyo, afadhali uachane nao. Kwa hiyo, nikamwombea, akapata kuona. Loo, jamani!

202 Kesho yake, maskini mwanamke mmoja alikuwa kwenye ofisi ya daktari, mtoto wake mchanga alishikwa na nimonia huko nje kwenye mvua hiyo, na maskini mama, akaenda kwa daktari pamoja naye, nimonia mbaya sana, naye akafa asubuhi hiyo saa tatu ofisini mwa huyo daktari. Basi usiku huo saa nne na nusu, alikuwa amesimama kwenye mvua hiyo, amesimama huko nje akijaribu kumwingiza mtoto huyo ndani apate kuombewa, baada ya kufa asubuhi hiyo.

203 Sasa, haya yameandikwa kwenye taarifa zilizotiwa sahihi na daktari. Jarida la Wafanyabiashara Wakristo liliyaandika. *Sauti* ya Wafanyabiashara Wakristo liliandika hiyo makala hivi majuzi tu. Pengine mmeisoma. Na hivyo, lakini kufanya hati. . . kutoa tamshi kama hilo, a—afadhali liwe limehatifishwa vizuri, kwa sababu wanaweza kukuingiza taabuni juu yake. Kwa hiyo, mambo haya ni ya kweli.

204 Na huko usiku huo, Billy akanijia, akasema, "Baba, jamaa huyo aliyesambaza kadi za maombi, alisambaza zote, nao wana maskini mwanamke mmoja amesimama pale," kasema, "Nina mabawabu mia tatu hapa, nao hawawezi hata kumshikilia," kasema, "anapitia mbio kati ya miguu yao na kila mahali." Alikuwa aking'ang'ania. Alikuwa Mkatoliki pia, kwanza kabisa. Naye huyo hapo.

205 Na kwa hiyo, baada ya kitambo kidogo, nikasema, "Vema, Ndugu Jack Moore," nikasema. . .Wengi wenu mnamjua Ndugu Jack Moore, nikasema, "wewe shuka ukamwombee huyo

mwanamke, yeye hanijui, jamani, hajawahi kuniona, watu wengi sana waliosongamana namna hiyo."

206 Nami nikasema, "Nilipokuwa nikizungumza, imani. . . " Nami nikatazama, na mbele yangu alikuwa amesimama mtoto mchanga kibogoyo hapa, mtoto mdogo wa Kimeksiko akinitazama, akitabasamu, ono. Nikasema, "Ngoja kidogo. Waambie hao mabawabu warudi nyuma wamwambie huyo mama aje hapa." Hii hapa Biblia yangu, sina budi kukutana na Mungu siku moja. Hiyo ni kweli.

207 Na kwa hiyo, wakamleta huyo mtoto mchanga jukwaani, akaanza kupaza sauti, "Padre, Padre!" Inamaanisha "baba," mwajua. Nikamwambia. . .Ndugu Espinoza, "Mwambie asimame." Alikuwa na blanketi iliyomfunika huyo mtoto mchanga, ikidondoka maji, nywele zake zimening'inia chini, maskini mwanamke mzuri sana, aliyeonekana mtanashati. Naye—naye akakimbia huku akipiga kelele namna hiyo, naye mtoto wake mchanga. . .

208 Nami nikaenda tu, nikaweka mikono yangu juu ya huyo mtoto mchanga, nikasema, "Baba wa Mbinguni, kama ono hilo lilikuwa ni Wewe ukiniambia nimwombee huyu mtoto mchanga, sijui, bali ninaweka tu mikono yangu juu yake kuomba, katika Jina la Yesu Kristo." Basi niliposema hivyo, huyo mtoto mchanga akasema, "Waa, waa," akaanza kurusha mateke namna hiyo na kuruka-ruka, na huyo hapo huyo mtoto mchanga.

209 Nami nikasema, "Ndugu Espinoza, weka mtu fulani na mwanamke huyo sasa, wala kamwe usiyaandike hayo, kuyaweka hayo kwenye—kwenye shuhuda, hadi daktari asaini taarifa." Kwa hiyo kesho yake, walikuwa wametuma mkimbiaji, akaenda na daktari, daktari, akamtazama huyo mtoto mchanga, akasema, "Nilimchunguza mtoto huyo mchanga na kutangaza amekufa, alikufa kwa nimonia asubuhi ya leo, kupumua kulikoma, kila kitu, ofisini mwangu saa tatu." Akatia saini jina lake namna hiyo.

210 Nayo hiyo hapo, huyo mtoto mchanga alikuwa akiishi kwa sababu maskini mama mdogo aling'ang'ania. Kanisa Katoliki ama si kanisa katoliki, ama chochote kile ambacho kilikuwa kikijaribu kumzuia, alikuwa. . .alimwona yule kipofu akifunguliwa macho yake usiku uliotangulia, naye akang'ang'ania. Kwa nini? Alijua kama Mungu angeweza kuyafungua macho ya huyo kipofu, Mungu angeweza kuchukua. . .?. . .Mungu yeye yule anayeyafungua macho ya vipofu anaweza kurudisha uhai, kwa sababu Yeye ndiye Mrejeshaji wa uhai. Bila shaka. Aliamini. Aling'ang'ania.

211 Mungu turehemu. Hivi hatuwezi kung'ang'ania alasiri hii, ku—kumfikia Yesu Kristo? tunapomwona akija moja kwa moja katikati yetu namna hii, na kufanya mambo ambayo hayajawahi kufanywa tangu siku za mitume. Kwa nini tusiweze

kung’ang’ania na kujisukumiza ndani? Hakika, kama imani yetu kamwe ikishikilia, na kweli tumeshawishika kwamba ni Mungu, tutang’ang’ania.

212 Asanteni. Wakati wangu wa kuondoka umewadia, nami ninataka kuwaombea wagonjwa wote. Siwezi kuleta mmoja baada ya mwingine jukwaani na kuwaombea chini ya ono, kadiri ya maono manne ama matano nao wangenibeba wanitoe nje. Mnajua hilo. Ni wangapi wanaoelewa hilo? Biblia inafundisha hilo. Yesu, ya kwanza...maskini mwanamke yule aligusa vazi Lake, ono la namna hiyo, Naye akasema, “Naona ya kuwa nguvu zimetoka, nikawa dhaifu.” Kwa hiyo, mimi...Mnajua mimi... kwamba hatungeweza kustahimili hilo.

213 Lakini je, mnaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, Naye alitufundisha, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya. kazi nizifanyazo Mimi hao nao watazifanya,” na kadhalika? Aminini hayo kwa yote yaliyo ndani yenu, naye Mungu atawatuza kwa yale mnayoomba yafanyike. Mnaamini hilo?

214 Sasa, kabla hatujapangisha mstari wa maombi humu jengoni, nataka uchaji wenu kwa muda kidogo. Aminini. Wakati mwingine lazima ukate kama kila kitu kwa Neno, lakini, nitakapokutana nanyi kwenye siku ya hukumu, hakutakuwa na damu ya mtu yeyote juu yangu. Mnaona? Nataka mjue ya kwamba ninawaambia Ukweli moja kwa moja kutoka katika Neno. Na endapo Mungu hatathibitisha ukweli huo, basi si Kweli, si Mungu. Kama Mungu akiithibitisha Kweli hiyo, basi ni Kweli, nanyi mwisikilize.

215 Kabla sijashuka huko kwenda kuwawekea wagonjwa mikono, nataka baadhi yenu hapa mwamini kwa moyo wenu wote kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ni Mwana wa Mungu kadiri alivyowahi kuwa, na ni Roho Wake, nami ninawaambia jambo hili, na Hili ndilo Neno Lake. Mnaamini hilo? Asanteni kwa imani yenu.

216 Sasa, ili nipate kuwa na hakika upako wa Bwana u juu yangu, kabla hamjaondoka kwenye viti vyenu, nawatakeni mseme, “Bwana Mungu,” moyoni mwako, namna hii, “Najua mtu yule anayesimama pale hanijui, ninajua, amenithibitishia hilo katika siku hizi mbili usiku ambazo amekuwa akihubiri, ya kwamba Wewe uliahidi mambo haya katika siku za mwisho, naye asiyeamini anayaondokea, lakini nitaninii...Mimi ni mwaminio, Bwana, ninaamini. Jalia niguse upindo wa vazi Lako, Wewe ujibu kupitia mhubiri yule pale juu, na ufanye kazi ile ile uliyofanya ulipokuwa hapa duniani kupitia Kanisa Lako, nami nitajua ya kwamba mimi ni mshiriki wa Kanisa hilo, kwa maana kwa Roho mmoja nimebatizwa katika Mwili huo.” Naam, ndiyo. Wewe sema hivyo, na uamini.

217 Sasa, kila mtu awe na kicho kwa muda, na akae kimya kwa muda kidogo. Mungu awabariki. Nisipoweza kuwaona, kama ikitokea Roho aniguse, sitaweza kuwaaga kabla sijaondoka, sitasema kwaheri, nitasema neno la Kijerumani, "Auf Wiedersehen," hiyo inamaanisha, "Tutakutana tena." Tutakutana tena mahali fulani, ikiwa si hapa, ng'ambo ya mto, tutawaona ng'ambo hiyo. Nitakaposimama huko kwenye Siku ya Hukumu, na siku hii iangaziwe kwenye skrini ya hukumu ya Mungu kule, mtaona nimewaambia ukweli. Nimekuwa mwaminifu kwenu, sijazuilia lolote; nimeliweka tu jinsi Neno linavyosema, na hilo hapo.

218 Sasa, Mungu Mwenyezi, njoo jukwaani, na jalia watu hawa wajue ya kwamba mtumishi Wako hayuko hapa kwa kusudi lingine, ila ni kwa sababu Wewe uliagiza. Sasa, Baba, nimenena habari Zako, Wewe nishuhudie, ya kwamba nimesema kweli. Katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba haya.

219 Sasa, mwaminini Mungu, msitie shaka. Vema sasa, angalieni huku juu, na mwamini. Aminini, tafadhali. Moyoni mwako kuwa ukisema, "Bwana, Mungu . . . " Omba tu. Ona kama Mungu anaweza kuniambia kile unachoomba, angalia kama ni Roho Mtakatifu au siye.

220 Jamaa huyu mdogo hapa mwisho, aliyeketi hapa mwishoni mwa safu ya mbele hapa, aliinamisha kichwa chake, akaendelea kuomba. Anaomba, anajaribu, anamwomba Mungu amwondolee pumu hiyo. Ikiwa unaamini . . . Je, hiyo ni kweli? Inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Vema, wewe . . . imekuacha sasa hivi. Amina. Kwa hiyo sasa, kama si yeye yule jana, leo, na hata milele, Yesu Kristo ni nini? Hiyo ni kweli?

221 Mwangalie mtu huyu anayeketi hapa nje, akinitazama, anamwombea shemeji ambaye ni mahututi sana, sana. Hiyo ni kweli. Kama unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kupata kile unachoomba. Amina. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Mnaona Yeye yuko hapa. Je, hamjui hilo?

222 Mwangalieni huyu mama anayeketi hapa, kidogo ni mama mkongwe anayeketi hapo, anaomba, kwa sababu ana tatizo kwenye shingo yake, maumivu na kadhalika yanaendelea kupitia shingoni mwake, yakimsumbua. Hiyo ni kweli, mama, sivyo? Kama hiyo ni kweli inua mkono wako. Vema, pokea uponyaji wako. Nenda, ukaponywe.

223 Mnaona Yeye yuko hapa? Mnaamini hivyo? Sasa, hivi huwezi kung'ang'ania kusimama hapo na kusema, "Kama Uwepo wa Yesu Kristo uko hapa na unajua siri ya moyo wetu . . . "?

224 Nayo Biblia ilisema ya kwamba, "Neno la Mungu ni, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, na Mtambuzi wa mawazo ya moyo." Hilo lingewezaje kuwa Neno la Mungu? "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu," nilibatizwa katika Mwili Wake, Neno Lake linakaa *humu* ndani, "basi ombeni mtakalo,

nanyi mtatendewa." Amina. Kwa nini hatuwezi kung'ang'ania, kuamini kwa moyo wetu wote?

225 Ni wangapi wenu ninyi watu humu ndani mlio na kadi za maombi, huku katika mstari huu hapa, na mnataka kuombewa? Inua mkono wako. Vema. Ni wangapi ambao hawana kadi za maombi na wanataka kuombewa?

226 Jambo lingine, ni wahudumu wangapi waliopo hapa leo hii, ambao ni watu watauwa wanaoamini katika uponyaji wa Kiungu? Sikuulizi wewe ni wa dhehebu gani sasa, unaweza kuwa wa dhehebu lolote unalotaka. Lakini, unaamini katika uponyaji wa Kiungu, nawe unavutiwa na Mungu kuwaponya watu, kujaribu kufanya maisha kuwa bora ki—kidogo kwao, kuwapunguzia maumivu wanapokuwa safarini, nanyi mnaamini katika uponyaji wa Kiungu, inua mkono wako, wahudumu. Vema. Nitawaomba mje hapa na kusimama, na kupanga mstari pamoja nami, ili nitakapoondoka, kwamba watu wataona kuwa si mimi, mna haki ya kuwaombea wagonjwa kadiri nilivyo nayo mimi, mtumishi yeyote wa Mungu aliyetawazwa na Mungu ana haki. Yesu alisema, "Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Ati nini? Wahubiri wanahubiri Injili kwa kila kiumbe.

227 Nataka wahudumu, waje hapa na kufanya mistari miwili papa hapa, nitasimama moja kwa moja kati yenu, papa hapa chini, tutawapisha wagonjwa na wanaoteseka papa hapa sasa.

228 Nao watu wanaokuja, unapokuja, usije kwa mmoja wetu, njoo ukitii, kama kwamba ulikuwa unaingia kwenye dimbwi la kubatizia, shuka uje, ndipo wahudumu hawa watakapoweka mikono juu yako, pamoja nami, uamini kwamba utaponywa na kupata afya.

229 Sasa, tunataka tu wahudumu, wahudumu wa Injili, wahudumu tu. Vema. Nawataka wafanye mistari miwili hapa, wakifanya kitu kama kichochoro kati yao, njia ndogo katikati yao, wahudumu wa Injili. Asanteni, ndugu zangu, kwa ushirikiano wenu mzuri, nyinyi ndio walio bora sana, ninawathamini kama ndugu zangu, dada katika Kristo. Sasa, kumbukeni, mnavutiwa na watu hawa kuponywa, nanyi mmekuja kuonyesha imani yenu katika Mungu, ya kwamba mnaamini, na kuamini ya kwamba uponyaji wa Kiungu ni wa kweli. Na sasa, mimi . . .

230 Kila mtu hapa, ambaye ni mfuasi wa makusanyiko haya, anapaswa kujivunia mhudumu wao, tunapaswa kuwa na shukrani kwa ajili ya mtumishi ambaye atasimama hapa na kumwakilisha Kristo katikati ya ubishi na angali anaamini jambo hilo, kwa sababu wanajua ya kwamba Mungu yeye yule

wanayempenda na kumtumikia, Yeye Ndiye aujuaye moyo. Na wakati wowote unapokuwa mgonjwa, baada ya haya, ama jambo lingine, mchungaji wako ana haki ya kukuombea.

231 Je, mnampenda Mungu? Vema. Sasa, ninamtaka Ndugu Roy Borders aje hapa kwenye maikrofoni. Nami nitashuka hapo miongoni mwa watu, ataliongoza hili kusanyiko, jinsi ambavyo hawana budi kupitia mstarini. Ninyi watu mtaanzia upande huu, mkipitia moja kwa moja, huku wahudumu wakiwaombea, wakiwawekea mikono, halafu safu hii hapa, atawaambia jinsi ya kutoka na kusogea karibu. Njoni kwa njia moja ili tusichanganyikane, na kila mtu anayetamani kuombewa apate kuombewa.

Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Sasa, ndugu zangu wahudumu, ombeni kwa moyo wenu wote.

232 Baba yetu wa Mbinguni, tujalie hili sasa, ule wakati mkuu umewadia. Nimefanya vizuri sana niwezavyo, Bwana, kujaribu kuwaonyesha watu, ya kwamba, katika Biblia watu waliong'ang'ania ndio waliopata baraka za Mungu, kwa sababu waliamini, walikuwa na ahadi, waliiamini hiyo ahadi na wakaitii hiyo ahadi, wala hakuna kitu kilichowazuia nayo.

233 Sasa, Baba mwenye neema sana, watu hawa wametulia alasiri ya leo, hawa walio humu ndani, wamesikiliza kwa sababu wana sababu, wamekuja kutafuta rehema Zako. Umeonekana mbele yetu katika matukio makubwa, na kuonyesha kwamba Wewe ungali ni Yesu na kwamba Wewe uko hapa.

234 Nalo kanisa linapokea onyo lake la mwisho. Baba Mungu, najua hilo limepita juu ya watu tena na tena na tena, wamelisikia, lakini wakati mmoja watalisikia kwa mara ya mwisho. Tunajuaje kuwa haitakuwa leo? Kunao watu wanaoketi hapa leo hii, labda watu wamekuwa humu ndani leo, ambao watakuwa wamekufa kabla ya asubuhi. Jinsi sauti hizo zitakavyosikika masikioni mwao katika Umilele usio na mwisho huko ng'ambo! Jinsi wanavyoenda mbali na Kweli ya Mungu!

235 Loo, ninaomba, Baba, ya kwamba waaminio hawa wa thamani, waliopo hapa sasa, wataponywa, kila mmoja wao. Ninaomba ya kwamba watu hawa wa Mungu, watumishi Wako ambao. . .Una ofisi tano Kanisani, ulisema uliweka Kanisani, kwanza: mitume, kisha manabii, walimu, wachungaji, na wainjilisti. Mungu, uliwaweka Kanisani, labda hawawezi kutabiri na kusema mambo, labda hawana utambuzi, lakini wao ni watu walio walimu na wachungaji, mimi, ninapohubiri kwa bidii, wao wanasimama papa hapa kusema ni kweli, wanalitambua, wanaliamini. Mungu, waheshimu watu hao, waheshimu, yabariki makusanyiko yao, jalia uamsho wa mtindo wa kale uzuke katika kila mmoja wao, Bwana. Lijalie. Na uzichukue hizo Mbegu zilizokusudiwa tangu zamani ambazo

zimewekwa hapa kisiwani kabla haijachelewa sana. Tunajua utalijalia.

236 Sasa, tunaposhuka chini, heshimu maombi yao wanapoomba. Wanapoweka mikono yao juu yao, Bwana, mikono ya wahudumu ambayo imetengwa kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, naomba usikie na kuyajibu maombi; jalia kila mgonjwa anayepitia kwenye mstari huu, atoke kwenye mstari huu akimsifu Mungu kama Ibrahimu, "Itatukia kwa vyovyote vile, maana Mungu alisema hivyo." "Kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, naye Mungu atawainua. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya." Mungu alisema hivyo, na itakuwa, mtu fulani ataponywa. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaomba. Amina.

237 Ninamtaka mpiga kinanda, kama akipenda, ucheze kwa moyo wako wote, yote uwezayo, na kuufanya . . . Sasa, kusanyiko likiimba, "Amini tu, yote yanawezekana, amini tu." Ndugu Borders ataongoza sasa, kwenye mstari wa maombi. Mungu akubariki. [Ndugu Borders anatoa maoni. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

. . . yanawezekana, amini tu.

238 Nilikuwa nikiangalia mikono ikipita. Enyi watu, je, mmeniona nikiushika mkono wako, na kuuinua *hivi*? Mnakumbuka, ninyi Wakanada, mara ya kwanza nilipopata kuwaona, nami ningeweza tu kujua kwa kuweka mikono yangu juu ya mikono ya mtu huyo? Ni wangapi wanaokumbuka hilo? Kumbukeni, karama hii ilidhihirishwa kwangu kwa mara ya kwanza huku Canada, huko Regina, pamoja na Ndugu Ern Baxter usiku ule, nilipotabiri na kuwaambia ya kwamba Yeye aliniambia ya kwamba, siku moja, kama ningekuwa na kicho namna hii, kwamba—kwamba ningejua siri hasa za moyo wao. Ni wangapi wanakumbuka nikisema hivyo, miaka mingi iliyopita? Biblia ilisema, "Akiweko mtu miongoni mwenu wa kiroho au nabii, na anayosema yanatimia, basi msikieni." Nisikilizeni. Yesu Kristo anawapenda nyote. Nami niliangalia mikono hiyo ikipita, na asilimia kubwa yao tayari mtetemeko ulikuwa umewaacha kufikia wakati walipofika kwangu hapa, wakati hao wahudumu walipokuwa wamewawekea mikono, walikuwa tayari wameponywa kabla hata hawajafika kwangu.

239 Ndugu Byskal, Mungu akubariki. Nimekutambua tu hivi sasa, kwamba uko hapo, babake Ndugu Eddie. Mungu akubariki. Neema ya milele ya Mungu iwe nanyi daima hadi tutakapoona tena, na ndipo tungesema:

Hata twonane! hata twonane!

240 Hebu tuinue mikono yetu sasa. Niombeeni, nahitaji maombi yenu. Ninawapenda kwa upendo usiokwisha, ninapozungumza nanyi jinsi ninavyofanya, ni katika upendo, kwa sababu ninawapenda.

Hata twonane! (Mbarikiwe, ndugu. Mko sawa . . . Eddie) . . . twonane!
Mungu awe nanyi hata twonane . . . (Utaturuhusu tufumukane?)

241 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Nitamwomba Ndugu Eddie kama hatakuja hapa, na chochote kilicho moyoni mwake kusema. Nitaondoka hivi karibuni sana kwenda ng'ambo. Je, ninaweza kuwategemea ninyi kuniombea? Fanyeni hivyo. Kwa upendo wa kiungu, sitasahau Victoria, kukikumbuka kisiwa hiki. Mungu awabariki hata nitakapowaona tena. Ndugu Eddie.

62-0729 Anayeng'ang'ania
Curling Arena
Victoria, British Columbia Canada

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org